Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 176 | RAMADHAN 1434 AH | JULAI 2013 | WAFA 1392 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi za mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi, afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Mwenyezi Mungu Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito, na pia (Huwatakieni) mtimize hesabu na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa Amewaongozeni, na ili mpate kushukuru.(2:186)

Kiini cha Saumu Ramadhani "Kutukumbusha"

Asisitiza Kiongozi wa Ahmadiyya Duniani

Na Jamil Mwanga, Dar es Salaam

Katika moja ya hotuba ya Ijumaa ya hivi karibuni, Khalifa Mtukufu alizungumzia juu ya kiini cha Ramadhani, na alianza kwa kusoma aya zifuatazo:

'Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an kuwa mwongozo kwa watu, na Ishara zilizo wazi na mwongozo na kipambanuzi. Basi miongoni mwenu atakayeuona mwezi afunge saumu, na mwenye kuwa mgonjwa au yumo safarini, basi atimize hesabu katika siku zingine. Mwenyezi Mungu Huwatakieni yaliyo mepesi wala Hawatakieni yaliyo mazito, na pia (Huwatakieni) mtimize hesabu na kumtukuza Mwenyezi Mungu kwa kuwa amewaongozeni, na ili mpate kushukuru.' (2186)

Mwezi wa Ramadhani huja mara nyingi katika maisha ya Mwislamu. Mwislamu anafahamu ya kwamba ufunuo wa Qur'ani Tukufu ulianza kushuka katika mwezi huu. Mwislamu makini ambaye ana elimu anafahamu kwamba wakati wa maisha ya Mtume Mtukufu s.a.w kila mwaka wakati wa mwezi wa Ramadhani, Hazrat Jibril a.s. alikuwa akimsomea Qur'an (Mtume Mtukufu S.a.w) mara moja isipokuwa katika mwaka wa mwisho wa maisha yake ambapo Qur'an ilisomwa yote na alipata habari njema kwamba **'...Leo Nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendelea Islamu iwe dini yenu...'** (5:4).



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a)

Kwa mujibu wa Hadithi iliyosimuliwa na Hazrat 'Aishah (Allah awe radhi naye) katika Ramadhani hiyo ya mwisho Jibril a.s. alisoma Qur'an Tukufu mara mbili.

Qur'an Tukufu inao uhusiano maalum na mwezi wa Ramadhani. Kwa hakika, kila mwaka Ramadhani inatukumbusha kwamba Qur'an Tukufu iliteremshwa katika mwezi huu. Kiongozi wa Jumuiya ya Wailamu Ahmadiyya Duniani, Hazrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a) alisema atatolea maelezo kuhusu sehemu ya kwanza ya aya aliyoisoma mwanzo na siyo sehemu ya mwisho ya aya hiyo.

Kila mwaka, mwezi wa Ramadhani unatukumbusha kwamba Qur'an Tukufu ni kitabu cha mwongozo na kinatofautisha kati ya ukweli na uwongo kwa dalili zilizo wazi. Inatukumbusha kuhusu umuhimu mkubwa juu ya faida za kufunga saumu na jinsi mtu anavyotakiwa kufunga saumu. Ramadhani pia inatukumbusha kwamba mafundisho ya Qur'an Tukufu ni kamili na yenye maarifa mengi. Kwa hakika, ukumbusho huu unafaa tu iwapo tutaelewa siri na mantiki yake. Vinginevyo, Ramadhani inakuja kila mwaka na itaendelea kuja kila mwaka na itaendelea kutukumbusha masuala mbalimbali nasi tutafurahia kusikiliza ubora wake. Faida zake zitaeleweka pindi tutakapotekeleza kwa vitendo. Mara tunaposikia **Mwezi wa Ramadhani ambao imeteremshwa humo Qur'an...'** tunachukua Qur'an ili kuisoma. Malengo ya ukumbusho huu yatatimizwa pale tutakapojaribu kuelewa maana za Qur'an Tukufu ili

Endelea uk. 2

Mwisho mwema kwa Wamchao Rahman



Kutoka kushoto Bw. Saidi Manoro, Shk Abdul Karim Sharma, Shk. Abdul Wahab wakiwa katika picha ya pamoja mjini London mwaka 2008.

Na Mwandishi wetu

Ukiona mja katimiza aya ile ya Allah 'Kila nafsi itaonja mauti' na akapata sudi ya Khalifa wa zama kutamka kadamnasi 'Mwenzetu haikumpita sala ya Tahajudi', unahitaji ushahidi gani tena zaidi ya huu wa kuthibitisha ya kwamba mja huyo amefaulu? Na sifa hizi zote amezichuma Sheikh wetu kipenzi aliyetumia ujana wake wote akiwatumikia

Endelea uk. 3

Miaka 50 ya Kumbukumbu ya Sheikh Shaaban Robert

Mahmood Hamsin Mubiru
Dar es Salaam

Taifa letu limefika njia panda. Katu hatuwezi kuwatumikia mabwana wawili. Na mbinja mbili zilimpoteza mbwa msituni. Inatubidi tufanye uamuzi kuhusu lugha yetu azizi kwani siku zote ajizi nyumba ya njaa.

Hakuna anayekataa kuhusu umuhimu wa lugha ya Kingereza. Kwa hakika hakuna mwenye mushkili kuhusu lugha yoyote iwayo. Kila lugha ina thamani. Katu hatuna ugomvi na lugha ya Kiingereza na wala hatuna ubavu wa kukwepa historia. Sisi tulitawaliwa na Waingereza kama Muingereza alivyotawaliwa na Mrumi. Hakuna la ajabu katika hilo. Tunasikia ya kwamba Marekani nayo ilitawaliwa na Waingereza. Lakini baadae watawaliwa hao walisafisha tope hizo za kutawaliwa na wakajenga heshima yao, utu wao na taswira yao. Kwanini sisi hatuwezi kujifunza kutoka kwa hao? Kwanini sisi tunang'ang'ania kuwa wao? Kwa nini tuendelee kushikilia lugha yao hata mahala ambapo hapahusu?

Tatizo letu kubwa kama Taifa ni kwanini hatufanyi uamuzi wa busara na kuweka jambo hili bayana katika katiba yetu kuwa Kiswahili ndio lugha yetu ya Taifa na kwamba

Endelea uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

KWELIMASIHIAMEFIKA

Vuta vizuri hisia zako. Ni mwaka 1959. Siku tatu mfululizo fujo za kila aina za kuvunja sheria zinafanyika bila aibu, ni nafsi amara inayotawala. Wao wanaita kipindi hiki Vunja Jungu. Wanajidhatiti katika maasi, kwani wanaingia katika mwezi ambao wanafikiri upuuzi haukubaliki. Ni kosa kubwa lilioje, hakuna mwezi makosa yanapokubalika. Leo hivi jambo hili linafanyika lakini sio katika kiwango kile na linapigwa vita na wale wenye ghera juu ya Islam. Kwa hakika Masihi Amefika.

Kweli Masihi Amefika. Vuta tena fikra na ingia mwaka 1959. Niko Katoke maili takribani 30 kutoka Bukoba mjini. Tumetoka kwenye tarawehe. Tunakaa muda sio kumkumbuka Mwenyezi Mungu, bali ni karata na mazungumzo yasiyo kichwa wala miguu. Daku tayari, unajua saa ngapi hiyo! Hiyo ni saa nane juu ya alama. Tunapiga ubwabwa na kwenda zetu kulala. Hakuna cha kuamka Tahajudi. Leo 2013 nasikia kwa masikio yangu, nasikia tangazo katika msikiti wa karibu hapa Kiwalani Dar es Salaam, mwisho wa kula daku saa kumi na moja na dakika kumi (11:10). Natoa wito wa Allahu Akbar. Kijijini kwetu Katoke zingepigwa Astaghfirullah zisizo na idadi na kukulaumu kuwa umekula asubuhi na kukuuliza funga gani hiyo! Leo saa kumi na moja unaambiwa kula! Tena kwa kupitia kipaza sauti! Kweli Masihi Amefika.

Kijijini kwetu Katoke asubuhi hakuna kupiga mswaki! Si umefunga? Hata kupitisha maji mdomoni utafungulia saumu. Kana kwamba hiyo haitoshi, napita nikitema njia nzima. Chamno! Nipo katika saumu! Darasani kwetu ni patashika. Kila mara naomba ruhusa niende nje kutema mate nisije kufungulia saumu! Na shule yetu ilikuwa na walimu wavumilivu na kila ukiomba ruhusa unaruhusiwa kwenda nje. Hivi leo kupiga mswaki si kosa tena. Kutema hovyo utachekwa na kila mtu. Achilia mbali kutema hata ukila kwa bahati mbaya. Unaambiwa Aliyekulisha ni Mwenyezi Mungu. Tizama dini ilivyofanywa kuwa rahisi. Kweli Masihi Amefika.
Wala usilete swala la kuumwa. Mtu anatetemeka na ile baridi ya Bukoba, huku amejifunika Blanketi zito. Lakini jambo moja eti kafunga. Utakulaje wakati kila mtu amefunga? Utakuwaje kobe la mchana? Kwanza atakupikia nani! Basi unakwenda hivyo hivyo huku ukivunja maagizo yote ya Qur'an Tukufu yanayohusu saumu. Leo afadhali ukiumwa unakwenda hospitali unakula vizuri upate afya. Na penye udhuru unalipa fidiya. Kweli Masihi Amefika.

Kwanza Mwezi wa Ramadhani mtu atakujua umefunga kwa hivyo vituko na mbwembwe zake. Uso wako unaonesha kuchoka. Utakosaje kuchoka nawe umekula daku saa nane usiku? Basi hutaki kufanya kazi. Nguvu unazo? Kutwa kwenye karata. Na sikumuona hata mmoja aliyejishughulisha na usomaji wa Qur'an Tukufu. Tizama tuliyo nayo hivi leo! Funga ni baina yako na Mola wako, hakuna haja ya kumuonesha mtu yeyote mwingine.

Kweli kila mtu anashuhudia kuwa huu mwezi iliposhuka Qur'an Tukufu. Ukiingia msikitini kila mtu na msahafu wake anasoma. Mashindano ya usomaji wa Qur'an Tukufu imekuwa ada wakati wetu huu wa elimu. Na hiyo ni katika kutimiza 'Fasta bikul Khairati' -Shindaneni katika mema. Kweli Masihi Amefika!

Watu wanapigana vikumbo kisa anahara ya kwenda kufuturu. Basi mwenye Baiskeli unamuona mbioo! na huyo anayetembea kwa miguu anapiga hatua. Watu wa leo wameelewa. Kufuturu ni jambo rahisi sana. Mfukono mtu anabeba tende zake za shilimi 100, au karanga za shilingi 100 na ikitolewa adhana ya Magharibi bila bughudha anakaa chini, palipo na kiti anakaa juu ya kiti au ardhi ya Mwenyezi Mungu na afafungua saumu. Imetosha na ni sahihi. Mwenyezi Mungu Anawatakia yaliyo mepesi, wala Hawatakii yaliyo mazito. Mpaka tumeielewa vizuri aya hiyo! Kweli Masihi Amefika!

Dalili zote hizi ukiziona unasubiri nini kumpokea Masihi Aliyeahidiwa? Wewe unabaki ah! Umefikishiwa ujumbe wakati Mtukufu Mtume Muhamamd s.a.w. alisema hata kama ni kutambaa kwenye theluji lazima utambae ili kwenda kufanya baiat kwake. Na unapofika ameagiza umfikishie salamu. Wewe umemsikia mbona hujatoa salamu kama alivyokuagiza mtume s.a.w. Masihi Aliyeahidiwa a.s. anakukaribisha:

Naapa kwa jina lake, Mola Asiye ajizi,
Kuwa ni amri yake, mimi nifanye ulinzi,
Ubashiri nipeleke, ufunuo huu wazi,
Kiukeni kuta hizi, mwingie mwangu nyumbani.

Kiini cha Saumu ya Ramadhani

Kutoka uk. 1

maneno **'…kuwa mwongozo kwa watu…'** yawe yenye kueleweka vyema kwetu.

Ukumbusho kuhusu uhusiano kati ya Ramadhani na Qur'an Tukufu utaeleweka vyema kwetu pale tutakapojaribu kufanya juhudi maalum katika mwezi huu katika kuzingatia amri za Qur'an. Ramadhani inatukimbusha, kuzingatia amri zilizopo katika Qur'an na kutekeleza kwa vitendo na kuzifanya amri hizo ziwe sehemu ya maisha yetu. Kulingana na mafundisho ya Qur'an Tukufu, Ramadhani inatukumbusha kujikita katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu, kwa kusali sala zetu ipasavyo, kwa wakati na kutafuta radhi ya Mwenyezi Mungu na pia kwa kusali sala za nafali kwa unyenyekevu na kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Majukumu haya hutusogeza karibu na Mwenyezi Mungu na Humfanya awe karibu nasi na hivyo umbali kati ya mja na Mwenyezi Mungu huondolewa.

Ramadhani inatukumbusha kushikamana na kamba ambayo kwa upande mmoja imeshikwa na Mwenyezi Mungu na upande wa pili Ameining'iniza ardhini kwa ajili ya wale ambao wanatafuta ukaribu Naye. Yule anayeishika atampata Mwenyezi Mungu.

Ramadhani inatukumbusha kwamba Mwenyezi Mungu anasema: **'…Mimi Nipo karibu…'** (2:187). Tunatakiwa tuongeze kiwango cha ibada yetu ili kunufaika na haya.

Ramadhani inatukumbusha kutekeleza haki za watu na viumbe wa Mwenyezi Mungu zaidi kuliko hapo kabla. Kwa hakika, Mwenyezi Mungu anatukumbusha hata kuhusu haki za wengine, kama ilivyo haki kwa Waislamu, Anasema: **'…wenye kuhurumiana wao kwa wao…'** (48:30).

Watu wengine husahau haki za wale wanaowahusu; kwa hakika wengine husahau haki za ndugu wa damu. Hazrat Khalifatul Masih (a.t.b.a) wakati mwingine hupokea barua kutoka kwa mabinti wakieleza kuwa wazazi hubagua kati ya watoto wa kiume na mabinti. Wakati mwingine pindi urithi unapogawanywa na wazazi wakati wa uhai wao, familia nyingine huwanyang'anya (urithi) mabinti na kuugawa wote kwa watoto wa kiume. Ili kufunika uovu huo, huwauliza mabinti kama wana pingamizi lolote ambapo mabinti hukubali kwa kuhofia kuwafedhehesha, na wazazi wanafikiri kwamba wametenda haki. Hii sio haki bali ni dhambi na ni kinyume na maagizo ya Qur'an Tukufu. Inashangaza kwamba kuna baadhi ya wazazi siku hizi ambao hawatendi haki kabisa. Aidha, ni jambo jema kwamba wapo baadhi ya mabinti siku hizi ambao hujitolea na kuziacha haki zao kama sadaka ili kuwafurahisha wazazi wao. Hata hivyo, wanatakiwa wakumbuke kwamba kama kujitolea huko si kwa nia ya kweli, basi wanawafanya wazazi wao wapate dhambi kwa vitendo hivyo. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema kuwa anachowaambia tena wazazi hawa katili ni kwamba wamwogope Mwenyezi Mungu,nawalenduguwakiume ambao wamepita kiasi katika ubinafsi na huwashinikiza wazazi kuwakabidhi mali huku wakiwanyang'anya dada zao basi wajue kwamba wanayajaza matumbo yao kwa madonge ya moto.

Akirudia somo ambalo Ramadhani inatukumbusha, Hazrat Khalifatul Masih alisema kuwa tunapoingia katika mwezi wa Ramadhani inatufundisha kuwa kufuatana na mafundisho ya Qur'an Tukufu, kila mwislamu ajenge ari ya kujitolea. Tunatakiwa tujichunguze kuhusiana na ahadi ambayo tumeifanya kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Jumuiya Yake kwa ajili ya Ukhalifa wa Kiahmadiyya kujitolea maisha yetu, mali na muda. Tunatakiwa tutekeleze ahadi na kupima ni neema kiasi gani tuliyonayo katika kutimiza ahadi hii, na kuangalia amri za Qur'an katika hili na pia kuangalia amri hizo zinavyoagiza kuhusiana na kumtendea kila mmoja.

Ramadhani pia inatukumbusha kuhusu mahangaiko aliyoyapata Mtume Mtukufu (S.a.w) katika kuuokoa ulimwengu dhidi ya maangamio na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Na jinsi alivyomwomba sana na kumlilia Mwenyezi Mungu kuhusiana na hili, na kwamba nini tunatakiwa kufanya kutimiza haki hii.

Ramadhani imekuja kutukumbusha kuhusu kazi ambayo kwayo Mwenyezi Mungu alimpa bwana wetu, Mtume Mtukufu (S.a.w) katika pango la Hira and kisha akamtaka aitekeleze nje ya pango hilo na ni jinsi gani tunatakiwa tufanye kazi ya kueneza mafundisho kulingana na maagizo yake na mfano wake mwema. Ni kwa namna gani kwa hakika tunatakiwa tufuate maagizo ya kueneza Umoja wa Mwenyezi Mungu na ujumbe wa Islam na kuusambaza kote ujumbe wa **'…kuwa mwongozo kwa watu…'**

Ramadhani inatukumbusha kwamba tuwe wenye kutanguliza dini mbele ya dunia kama tunatafakari hali ya ibada (upweke) aliyokuwa nayo Mtume Mtukufu (S.a.w) katika pango la Hira.

Ramadhani inatukumbusha kwamba kama tunadai kumpenda Mtume Mtukufu (S.a.w) tunatakiwa tuufuate na kuuiga kila mfano wake mwema.

Mwezi huu umekuja kutukumbusha kutafuta ni jinsi gani Masahaba wa Mtume Mtukufu (S.a.w) walifikia cheo ambacho kwacho wanastahili kupewa heshima ya 'Allah awe radhi nao'. Kwa hakika, Masahaba pia ni mfano bora kwetu.

Mwezi huu pia unatukumbusha maisha ya Mtukufu Mtume (S.a.w). Ni kweli, hatuwezi kurudia zama hizo lakini tunayo mafundisho ya Qur'an Tukufu kama yalivyoteremshwa awali ambayo yanatufanya tutambue na kuthamini zama hizo.

Mwezi huu umekuja kutukumbusha ili tuuambie ulimwengu kwamba mafundisho ya Qur'an Tukufu pekee yanahusu kueneza amani na mfano mwema wa Mtume Mtukufu (S.a.w) ndio utakaoeneza amani duniani.

Mwezi huu umekuja kutukumbusha kwamba Qur'an Tukufu ni kitabu ambacho kimetoa amri zake zote kwa hoja, kwa hiyo kinatakiwa kisomwe kwa tafakuri makini ili tuwe miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu amesema: **'Wale tuliowapa kitabu wakakisoma kama ipasavyo kukisoma…'** (2:122). Yaani, wanatimiza haki ya kukisoma kama inavyopasa kukisoma, wanatafakari kama inavyopasa kutafakari na wanatimiza haki ya kile wanachokisoma, wanasikiliza na wanatafakari. Kama hatutafuata hili, basi madai yetu ya kuwa Waislamu ni ya maneno tu na tutahesabiwa miongoni mwa wale ambao Mwenyezi Mungu amesema: **'Na Mtume atasema: Ee Mola wangu, hakika watu wangu wameifanya Qur'an hii kuwa *kitu* kilichoachwa.'** (25:31)

Endelea uk. 3

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jumuiya, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jumuiya Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Kiini cha Saumu ya Ramadhani "Kutukumbusha"

Kutoka uk. 2

Wakati mwezi huu ukitupatia habari njema pia unatupa majukumu mengi, unatufanya tupime ni kwa kiasi gani tunatekeleza kwa vitendo mafundisho yake na ni kwa jinsi gani tunatenda ili kutuliza hofu ya Mtume Mtukufu (S.a.w). Vinginevyo, si Qur'an wala Ramadhani itakayokuwa yenye faida yoyote kwetu.

Mwenyezi Mungu ametoa maagizo lukuki kuhusu jinsi Anavyotaka mtu awe muumini wa kweli, na katika zama hizi tunakumbushwa kufanya mabadiliko kupitia kwa Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake). Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alisema ameelezea kwa kifupi masuala ambayo Ramadhani na Qur'an Tukufu vinatukumbusha, lakini Qur'an inayo mamia ya amri ambazo zinatakiwa kuzingatiwa na kutekelezwa. Hili haliwezi kufikiwa pasipo rehema ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anasema rehema Yake inaweza kupatikana kwa njia ya Sala. Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) alipenda kuelezea maagizo mawili kati ya mamia yaliyomo kwenye Qur'an Tukufu kwa sababu ni ya muhimu mno kuhusiana na uhusiano na amani katika jamii, ambayo ni katika kutafuta ukaribu na Mwenyezi Mungu kwa kutii amri Zake.

Kwanza ni unyenyekevu ambao kwa hakika ndio suluhisho la matatizo mengi. Mwenyezi Mungu amefanya unyenyekevu kuwa moja ya sifa za watumishi Wake wanaomwabudu Yeye na wanatafuta fadhili za Rahmani. Mwenyezi Mungu anasema: '**Na watumishi wa Rahmani ni wale wanaotembea ardhini kwa unyenyekevu…**' Mwenyezi Mungu pia anasema: '**… hakika Mwenyezi Mungu Hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye.**'(31:19). Haiwezekani awepo mtu ambaye kwa upande mmoja anakubali kumwamini Mwenyezi Mungu na kwa upande mwingine anasema hajali kuhusu kumpenda Mwenyezi Mungu. Kwa hakika, mtu mwenye busara na akili hawezi kusema hivyo. Hata hivyo, tunashuhudia kuwa chanzo cha matatizo ya kila siku ni majivumo na kiburi. Mtu ambaye hana kiburi na kwa hiyo pia sio mbinafsi yeye hupata ufaulu. Kiburi huleta ukaidi. Siku hizi masuala mengi hufikishwa kwa Khalifa Mtukufu (a.t.b.a) na mengi kati ya hayo hayapati ufumbuzi kwa sababu kiburi, ubinafsi na ukaidi inakuwa ni kikwazo cha kufikia suluhisho. Kama Mwislamu anahitaji mapenzi ya Mwenyezi Mungu, (na Huzur a.t.b.a anapotumia neno Mwislamu, kimsingi anawaambia Waislamu Wahmadiyya) mambo haya hayanabudi kuepukwa. Fadhila za Ramadhani zinapatikana pindi maagizo ya Qur'an yanapofuatwa. Ifahamike wazi kwa wale ambao migogoro yao ni ya muda mrefu kutokana na kiburi, migogoro hiyo kwa hakika chanzo chake ni kiburi na majivuno. Watu hawa wanatakiwa waoneshe unyenyekevu katika Ramadhani hii na watoe mkono wa suluhu na wajitahidi kuhesabiwa miongoni mwa Ebaadur Rahman (watumishi wa Rahmani) ambao hutembea kwa unyenyekevu na ambao huwa na shauku ya kupata mapenzi ya Mwenyezi Mungu hata kama kwa kufanya hivyo itasababisha kupata hasara za kidunia.

Pili, subira ndio ambayo ina uhusiano na unyenyekevu. Mwenyezi Mungu anasema '**Na ombeni msaada kwa subira na kwa Sala…**' (2:46). Ni nani huyo asiyehitaji msaada wa Mwenyezi Mungu katika kila hatua? Hata hivyo, Mwenyezi Mungu anasema kwamba wale wanaofanikiwa katika hili ni wale walio wanyenyekevu na kwa wengine hili ni jambo gumu sana. Anasema: '**… na kwa hakika jambo hili ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.**' (2:46). Inatakiwa kusali kwa subira na unyenyekevu. Kwa hakika, unyenyekevu ndio njia ya wale wanaotii amri za Mwenyezi Mungu, ni njia ya wale ambao humwabudu Mwenyezi Mungu. Msaada wa Mwenyezi Mungu huja wakati haki Zake zinapotimizwa kwa unyenyekevu sana katika kila hatua kwa maombi na subira na wakati ambapo mja humwelekea Mwenyezi Mungu. Vivyo hivyo, tafuteni nguvu ya kutimiza haki za watu kama Alivyoamrisha na muoneshe uimara na ustahimilivu na matokeo yake mtapata rehema ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu pia humsaidia yule aliye mnyenyekevu ili asipate hasara za kidunia, humsaidia dhidi ya maadui, humpandisha daraja kiroho na huleta amani katika fungamano za kijamii na hivyo rehema ya Mwenyezi Mungu inapatikana. Haya kwa hakika ndio matarajio ya mwaminio wa kweli na kwa hakika ndio anavyotakiwa awe.

Hazrat Khalifatul Masih (a.t.b.a) alisema tunatakiwa tujipime katika Ramadhani hii kulingana na jinsi alivyotueleza leo, tutafakari ni kiasi gani tumejiandaa kufanya mabadiliko na kupiga hatua katika hili. Vinginevyo, Ramadhani itakuja kila mwaka ilimradi tunaishi na tutakuwa tu tukisikiliza hoja za kielimu kuhusiana nayo. Umuhimu wa '**…kuwa mwongozo kwa watu…**' ni kwamba mtu azingatie mambo haya kwa makini.

Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake) anasema: 'Kumbukeni kwamba Qur'an Tukufu ni chemchemi ya Baraka na ni chanzo cha kweli cha wokovu. Wale ambao hawaifuati wanatakiwa wajilaumu wenyewe. Kundi la kwanza la wale ambao



Qur'an Tukufu ilianza kushushwa ndani ya mwezi wa Ramadhan

hawaifuati ni wale ambao hawaiamini na hawaamini kuwa ni Neno la Mwenyezi Mungu. Watu hawa wako mbali. Hata hivyo, inashangaza sana na ni bahati mbaya kwa wale wanaoamini kuwa ni Neno la Mwenyezi Mungu na ni ponyo bali hawaifuati. Wengi miongoni mwao hawaisomi katika maisha yao yote. Mfano wa watu ambao wameiacha na hawajali kuhusu Neno hili la Mwenyezi Mungu ni kama mtu ambaye anafahamu kuhusu chemchemi ya maji safi, baridi na matamu na anafahamu kwamba maji yake ni tiba na yanatibu kila maradhi. Anafahamu kwa yakini, lakini pamoja na kufahamu hilo na licha ya kwamba ana kiu na anaumwa maradhi mengi lakini hayaelekei maji hayo. Ni mjinga na mwenye bahati mbaya kiasi gani mtu huyu! Angalitakiwa kunywa kutoka kwenye chemchemi hii na kutosheka na kufurahia ladha ya maji haya yanayoponya. Pamoja na kufahamu bado anajiweka mbali nayo mithili ya mtu asiyefahamu na anaendelea kuwa mbali nayo hadi mauti yanapomkuta. Mtu huyu kwa hakika anastahili kuonywa na kuaswa.

Hii pia ndio hali ya Waislamu wa zama hizi. Wanafahamu kwamba Qur'an Tukufu ndio msingi wa mafanikio yote na unatakiwa ufuatwe. Lakini, hapana, hata hawaijali! ....Waislamu walitakiwa waizingatie, na pia ni muhimu sasa kwao kuzingatia chemchemi hii yenye Baraka kubwa na kuithamini. Kuithamini ni katika kuifuata. Kisha wataona jinsi Mwenyezi Mungu atakavyoondoa matatizo na tabu zao. Ikiwa tu waislamu wataelewa na kutafakari kwamba Allah amewaandalia njia iliyonyoka nao wanaipita ili kunufaika kwayo.' (Tafsiri kutoka Malfuzat, Sura ya 7, uk. 181-182).

Kama tu Waislamu wa leo, viongozi na jamii ambao wanauana wenyewe kwa wenyewe na kupoteza maisha ya mamia ya watu, wangaliifuata Qur'an Tukufu na kumkubali Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake) uovu huu ungetoweka. Mwenyezi Mungu awajaalie hekima waweze kufuata mafundisho ya Qur'an!

Masihi Aliyeahidiwa (amani iwe juu yake) pia ametuambia tuitafakari Qur'an Tukufu kwa vile imebeba mafundisho yote. Anasema: 'Ieleweke kwamba Qur'an Tukufu inabainisha dini ile ambayo hakuna pingamizi linaloweza kuelekezwa kwa sababu baraka na matunda yake ni mapya. Injili haifafanui dini kwa ufasaha. Mafundisho yake yalikusudiwa kwa ajili ya zama za wakati huo lakini kwa hakika hayafai kwa ajili ya kila hali na kwa zama zote. Tofauti hii inaihusu Qur'an Tukufu pekee kwamba Allah ametoa tiba kwa kila ugonjwa na ametoa maagizo mema kwa wenye akili. Aidha, uovu wowote uliokwishathibitika imeelezwa namna ya kuutokomeza. Hivyo, endeleeni kuisoma Qur'an Tukufu na endeleeni kuomba na jaribuni kuenenda kulingana na mafundisho yake.' (Imetafsiriwa kutoka Malfuzat, Sura 9, uk.122).

Ushauri huu pia unatuhusu; mtazamo wetu si tu kwa ajili ya kuwakosoa wengine. Sisi pia tunapaswa kuifuata na kutekeleza kwa vitendo mafundisho yake ili kuwa na mwisho mwema. Mwenyezi Mungu atuwezeshe kukifanya Kitabu hiki kikuu sehemu ya maisha yetu na kutupatia radhi Yake. Na ajaalie Ramadhani hii itupatie elimu kubwa ya Qur'an Tukufu. Amin.

Mwisho mwema kwa Wamchao Rahman

Kutoka uk. 1

watu wa Afrika Mashariki kwa mapenzi, unyenyekevu na huruma. Huyo si mwingine isipokuwa ni Maulana Sheikh Abdulkarim Sharma aliyefariki mwanzoni mwa mwezi mtukufu wa Ramadhani huko Uingereza. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Sheikh Abdulkarim Sharma mwana wa sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa alizaliwa Qadian - India, mwaka 1908 miezi michache baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa. Alitia nanga katika jiji la Dar es salaam tarehe 15/05/1948. Toka wakati huo hadi mwaka 1973 aliendelea kuwatumikia watu wa sehemu hii ya Afrika na kutokana na hali ya uzee akaenda kuishi London kwa binti yake hadi alipofariki mapema mwezi huu na sala ya jeneza kuongozwa na kiongozi wa Waaminio Khalifatul Masih - V Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba). Na sala ya ghaibu ilisaliwa pia Masjid Salaam - Dar es salaam, Msikiti aliyousimamia ujenzi wake hadi ulipokamilika na kufunguliwa mwaka 1957.

Jopo la waandishi wa Mapenzi ya Mungu limo katika harakati za kufanya utafiti juu ya maisha ya Mwanachuoni huyo na Inshallah katika toleo lijalo tutamtendea haki Sheikh huyo aliyeipenda sana Afrika Mashariki. Hivyo tunatoa wito kwa mtu yeyote yule aliye na picha, barua, masimulizi na chochote kinachomhusu Sheikh Abdulkarim Sharma awasiliane nasi ili tuweze kukamilisha kazi hii Inshallah.

TANZIA

Mzee Mohamed Sanduku afariki dunia.

Kwa masikitiko makubwa, Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania inatangaza kifo cha Mzee Mohamed Sanduku wa Kigamboni Dar es salaam. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea. Mzee Mohamedi Sanduku mwenyeji wa Kilwa, alijiunga na Jumuiyya miaka ya 1960 na kupata misuko suko kwa sababu ya imani yake. Katu hakutetereka. Ndugu na jamaa zake wote walielezwa juu ya imani yake, na hakuna aliyekuwa na wasiwasi ya kwamba yeye si Ahmadiyya. Ni jambo la kusikitisha sana kuwa ipo desturi kwa hivi sasa ndugu wa marehemu ambaye ni Ahmadiyya hung'ang'aniwa na kuthaminiwa akishakufa. Hapo hutaka wamuoshe wao, kumsalia na hadi kumzika. Na hivyo ndivyo walivyofanya kwa ndugu yetu marehemu Mohamedi Sanduku wa Kigamboni. Kwa hakika hiyo ni dhuluma kubwa kwa marehemu. Si mwenendo wa Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya kugombea maiti.

Ndugu yetu huyo alipofariki tarehe 27/07/2013 Jumamosi, huko nyumbani kwake Kigamboni Dar es salaam, Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya ilikwenda nyumbani kwa marehemu na kuomba isimamie shughuli zote zinazotakiwa kwa Marehemu, lakini ndugu zake walikataa kata kata, nasi hatukuwa na njia yoyote isipokuwa kufanya lile ambalo lilikuwa katika uwezo wetu nalo ni kumsalia sala ya jeneza ghaibu siku ya Ijumaa tarehe 02/08/2013.

Yarabbi Mola Wadudi,
Mpokee Mohamedi
Mfuasi wa Mahadi
Kwako apate tulia

Binadamu ni dhaifu
Hivyo penye upungufu
Tunakuomba Raufu
Makosa kumfutia.

بسم الله الرحمن الرحيم

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA - KALENDA YA MATUKIO KWA MWAKA 2013/2014

MWEZI	MWAKA	TAREHE	TUKIO
JULAI	2013	01 – 10	Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa – Dar es Salaam.
		10 – 16	Siku maalum za kukutana na viongozi wa serikali/waandishi wa habari sehemu walipo kwa lengo la kuleta uhusiano nzuri.
		15 – 21	Siku maalum za makusanyo ya michango ya Waqf-e-Jadid na Tahrik Jadid
		09	**Mwandamo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani**
AGOSTI	2013	1 – 8	Maonyesho ya Kilimo kitaifa - Mikoa husika
		1 – 8	Siku maalum za Makusanyo ya Eidul Fitri na Eid Fund
		09	**Sikukuu ya Eid Ul Fitri***
		30 – 31	**Jalsa Salana Uingereza**
SEPTEMBA	2013	1	
		1 – 10	Siku maalum za maonyesho ya vitabu katika Mikoa husika.
		06 – 13	Wiki maalum ya kuchanga mchango wa mkutano wa mwaka (Jalsa Salana)
		27 – 29	**Jalsa Salana Tanzania**
OKTOBA	2013	15	**Eid Ul Adhha***
		19 – 20	Uendeshaji wa semina za Tabligh katika kila tawi.
		26 – 27	**Siku maalum za mahubiri nchi nzima.** Mahubiri yafanyike, viongozi wote wa Matawi ni lazima washiriki, ripoti itumwe Makao Makuu.
NOVEMBA	2013	15 – 29	Ahadi za Tahrik-e-Jadid kwa mwaka mpya (Novemba 2013 / Oktoba 2014)
		17	Siku ya waanzilishi wa dini. (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
		24	Mitihani kutoka kitabu cha: **Zawadi kwa Kaisari**
DISEMBA	2013	02 – 16	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya Waqf-e-Jadid.
		14 – 15	Ijtimaa ya Ansarullah Kitaifa - Dar es Salaam
		21 – 27	Siku maalum za Tarbiyyat Kitaifa. (Msukumo uwekwe zaidi kwa Waahmadiyya wapya).
JANUARI	2014	13 – 26	Ahadi mpya za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2014.
		26	Mitihani kutoka Kitabu cha: **Ushindi wa Islam**
		24 – 31	Siku maalum za makusanyo ya mchango wa kawaida.
FEBRUARI	2014	03 – 09	Siku maalum za kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu.
		20	**Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		22 – 23	Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washriki, Ansar, Khuddam na Lajna).
MACHI	2014	01 – 09	Siku maalum za kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya 2014 na kuchagua wajumbe.
		16	**Siku ya Seeratu Nabii.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		15 – 16	Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki).
		21	Mahubiri ya tarehe 16-17 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote.
		23	**Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		31	Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2014.
APRILI	2014	06	Mitihani kutoka kitabu cha: **Nyota ya Kaisari**
		06 – 13	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik Jadid na Waqfe Jadid.
		26 – 27	**Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2014.**
MEI	2014	09 –16	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida).
		09	Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2014
		27	**Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
JUNI	2014	01 – 15	Siku maalum za kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe.
		20 – 22	**Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Kitaifa.**
		27 – 29	**Ijtimaa na Shura ya Lajna Imaillah Kitaifa.**

*Zingatia: Saumu ya Ramadhani, na Sikukuu zote mbili zinategemea kuandama kwa mwezi.

Miaka 50 ya Kumbukumbu ya Sheikh Shaaban Robert

Kutoka uk. 1

itatumika hivyo? Matamshi na maandiko mazuri yageuzwe kuwa vitendo. Kwani aja ya mja kunena muungwana ni vitendo.

Kama Taifa tunaonesha kutokuwa na shukurani kwa lugha yetu hii ya thamani. Imetufanyia mengi mno. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Aliyetujaalia Kiswahili kisemwe bara na Pwani kwacho Akatuunganisha wakazi wa jadi na walowezi waliohitilafiana makabila na rangi na dini, Akawawezesha viongozi kutumia Kiswahili kuwafungua watu akili, tukapambazukiwa na alfajiri ya utambuzi iliyofuatiwa na asubuhi inawirishayo kwa wingi wa miali na mwangaza kamili. Kwa Kiswahili wanyonge wakapata nguvu na ukakamavu wa kupambana na Serikali ya Kikoloni yenye mabavu. Wapo watu wengi duniani hivi leo wanatafuta kwa udi na uvumba wawe na lugha inayozungumzwa na watu wote katika jamii husika na bahati hiyo hawana. Kwa



Sheikh Shaaban Robert - Askari maarufu wa Kiswahili

nini sisi tunachezea lulu hii ya thamani? Kwa nini hatujali?

Wako wapi basi viongozi wanaojali Kiswahili? Yuko wapi kiongozi ambaye aliombwa na waongoza shule, shule hiyo iitwe kwa jina lake yeye akashauri ya kwamba kuna mtu aliyetoa mchango mkubwa kwa taifa hili afadhali mtumie jina lake na akasema mtu huyo ni Shaaban Robert. Yupo wapi kiongozi mwenye huba na mapenzi ya kuwaita Washairi Ikulu kuzungumzia mashairi na kupata kikombe cha tangawizi? Yupo wapi kiongozi aliyetumia wakati wake kutafsiri maandiko maarufu duniani ili nasi akina pangu pakavu weka mchuzi tumaizi fikra za watu wengine duniani?

Kweli tumehemewa! Shaaban Chuma Gonga mshairi maarufu kapita hivi hivi bila hata jani moja kutikisika. Aibu ilioje kwa taifa letu. Mwinyihatibu Mohamedi katawafu huko Tanga, hata neno moja la rambirambi halikutoka. Lakini aliwahi kukaribishwa Ikulu alipotunga utenzi juu ya uhuru wa Tanganyika. Tutaficha wapi uso wetu kwa dhuluma hiyo tuliyoifanya? Sihiyana Swalehe Mandevu Mtendamema kafariki hivi karibuni, hata chozi dogo la masikhara halikutoka! Utasemaje unajali Kiswahili? Utasemaje unaenzi Kiswahili? Nipe jina la kiongozi yeyote unayemfahamu aliyewahi kunukuu mmoja wa wazungupule wetu katika hotuba zake?

Ni dhahiri tumejikwaa na kuanguka. Lakini ukianguka hubweteki. Unajipangusa vumbi na kuanza safari tena. Na huu ndio wakati mzuri wa kuanza safari wakati tunakumbuka miaka 50 toka atawafu Shaha wa Malenga mahiri mtunga beti Shaabani wa Robert. Kwa heshima ya malenga wetu huyu tuanze sasa kutumia Kiswahili hadi chuo kikuu. Tuanze kuwaenzi waandishi wetu. Tuwatafutie mahali maalum pa kuwapumzisha. Tutafute siku maalumu ya kumbukumbu yao. Tuanze kuipa kipaumbele lugha yetu ya Kiswahili. Ni lazima tukumbuke kwamba yote tunayoyahitaji hivi leo amani, mshikamano, maelewano, kuvumiliana vyote hivyo haviwezi kukamilika bila ya Kiswahili. Tutafute kwanza ufalme wa Kiswahili na kila kitu kitaongezwa kwetu. Na hiyo labda ndio njia bora ya kumuenzi na kumkumbuka Shaaban Robert.

Shaaban Robert kumbukumbu iliyozirwa

Na Abdullah H. Mbanga

Ni miaka 50 imepita tangu pale Muandishi, Mzindushi na Muashi wa ushairi na Kiswahili Marehemu Sheikh Shaaban Robert alipofariki.

Juu yake kalamu n yingi za waandishi zimepata kumwaga wino katika kuelezea maisha yake. Jambo hili pia alikwisha lifanya mwenyewe kwa kalamu yake pale alipoitia katika hifadhi ya wino na karatasi simulizi aliyoiita *'Maisha yangu na baada ya miaka 50'*. Kwa hivi kumbukumbu la maisha ya Shaaban si jambo lililo adimika katika maandishi ya mjazo na hata katika ushairi. Hata leo tunapozungumzia miaka 50 baada ya kifo chake, tayair tuna fututu la waandishi anuwai wenyeji na wageni waliokwisha sawiru maisha ya nguli huyu wa Kiswahili.

Jambo linalohuzunisha sana ni hili la kwamba ni nusu karne tu imepita, tangu atutoke lakini harakati ya uendashi wa fikra na kazi zake zimekuwa adimu sana. Mipango ya kurithisha falsafa zake kwa vizazi vya sasa zimekuwa katika usiru mkubwa. Juu ya hayo hata lugha yenyewe ya Kiswahili aliyoitumikia katika maisha yake yote imeachwa ukiwani. Ushairi ambao yumkini Shaaban alikuwa tayari kuufia, sasa umekosa nafasi katika vikao vya wanaojinaki uungwana.

Watu kama Charles Dickens, William Shakespear, Bernard Shaw na wanalugha wengine katika nchi zao wamepewa umuhimu wa aina yake katika jamii zao. Kila mara maadhimisho ya siku zao yalifanywa. Kuna maeneo yaliyoandaliwa rasmi kwa ajili yao. Pia jamii na mataifa yao yametilia mkazo wa usambazaji kuendeleza na kuimarisha mashiko ya kazi zao.

Jambo la kuhuzunisha ni kwamba wakati picha ya mojawapo ya kazi za Dickens zipo katika noti za fedha za nchi, sisi jina wala picha ya Shaaban Robert kinachopewa taadhima yoyote katika mtazamo wa kitaifa. Na hivyo ndiyo maana hata kwa vijana wa leo Shaaban Robert bado linaweza kuonekana zaidi kuwa jina la Shule au la mtaa kuliko kuwa jina la nguli wa lugha ya Kiswahili.

Kwa neno zima ni vyema kwa jamii na taifa kwa ujumla likachukua hatua rasmi ya kuanza kuadhimisha, kuzitunza, kuzifufua na kuziendeleza harakati za Shaaban Robert ili kuhuisha hamasa ya lugha na utamaduni wetu katika jamii na taifa. Tumuenzi Shaaban Robert aliyekienzi Kiswahili ambacho kimetuenzi kwa dahari. Tuongeze bidii katika hili kwani; 'bei ni bidii ukitalii'.

Kuna Nini katika jina?

Na Mtafiti wetu

Mwandishi maarufu wa visiwa vya Uingereza William Shakespear aliwahi kuuliza; "Hivi kuna nini katika jina?" Jitihada yetu ya kujibu swali hilo asaa ikatusaidia tukayaelewa yale ambayo tulikuwa hatuyaelewi kuhusu mshairi na mwanariwaya wetu Shaaban Robert.

Ni desturi ya watu wa Pwani kutoa majina kwa watoto sawa na siku waliyozaliwa, ikitegemea na jinsia. Mtoto wa kiume akizaliwa siku ya Ijumaa anaitwa Juma, na binti anaitwa Mwajuma. Wa kiume azaliwapo Alhamisi huitwa Hamisi, na wa kike Mwanahamisi. Miezi pia inatumika kuwapa watoto majina. Mtoto akizaliwa mwezi wa Rajabu anaitwa Rajabu. Akizaliwa mwezi mtukufu wa Ramadhani anaitwa Ramadhani.

Kalenda ya Islam ina miezi ifuatayo; Mwezi wa kwanza unaitwa Muharram, wa pili Safar, wa tatu Rabbiul Awwal, wa nne Rabiul Thani, wa tano JamadulAwwal, wa sita Jamadul Thani, wa saba Rajabu, wa nane Shabani, wa tisa Ramadhani, wa kumi Shawwal, wa kumi na moja Dhul-Qadah na wa kumi na mbili Dhul-Hijjah.

Mwezi wa nane sawa na kalenda ya Islam ni Shaaban. Huu ni mwezi wenye utukufu wa aina yake. Na mtukufu Mtume Muhammad (saw) alifanya ibada sana na kufunga katika mwezi huu ili kukaribisha m wezi Mtukufu wa Ramadhani. Ni bahati sana unapojaliwa kupata mtoto katika mwezi huu wa Shaaban. Na ndivyo ilivyotokea kwa Mzee Suleiman Ufukwe na Bi. Mwanawema mwaka 1909 walipojaliwa kupata mtoto ambaye walimpa jina kwa kumbukumbu ya mwezi huo unaoukaribisha mwezi mtukufu wa Ramadhani. Hapana shaka jina la mtu hupata kuathiri pia vitendo na mwenendo wake na jina lina kuwa na maana maalumu katika maisha yake.

Robert ni jina ambalo limewatatiza wengi. Wengi hufikiri huenda baba yake Shaaban alikuwa Mkristo. Jina hili nalo lina historia inayotupa picha juu ya chimbuko la Shaaban. Babu yake Shaaban Mzee Kanduru alikuwa anafanya kazi kwa Mkuliwa wa Kiitaliano ambaye walishibana na kuelewana sana. Mkulima huyo aliitwa Robert. Kwa muda Mzee Kanduru hakujaaliwa kupata mtoto, lakini kama wasemavyo waswahili; 'Mungu si Athumani'. Mzee Kanduru akaajliwa kupata mtoto. Furaha ilikuwa kubwa kwa watani na hata huyu Mzungu Bwana Robert. Watani walimpa jina la Ufukwe kijana huyu aliyezaliwa. Baba mtu akampa jina Suleiman na yule Mzungu akasisitiza mtoto aitwe Robert. Taratibu Ufukwe na Suleiman yakasahaulika, lakini si kwa wanahistoria na watafiti. Hivyo Robert linanasibishwa na yule Mzungu aliyekuwa mkulima ambapo Bwana Kanduru alikuwa akifanya kazi.

Waliobobea katika elimu ya jamii, wanaweza kutueleza umuhimu na nafasi ya majina katika malezi ya watoto. Mtukufu Mtume Muhammad (saw) alieleza kwamba watoto tuwachagulie majina mazuri. Wahaya nao wana methali isemayo; *'Eibara libi liita nyiinalyo'* (Jina baya humuangamiza yule aliye na jina hilo). Mwanaharakati kutoka Kenya Profesa Micero akihutubia katika kigoda cha Mwalimu Nyerere alisema ya kwamba Wakikuyu wanaamini kwamba jina alililonalo mtu lina mchango mkubwa katika kutengeneza ramani ya maisha ya mtu.

Ni dhahiri basi kwamba Shaaban katika pande zote alibahatika sana. Baba yake aliitwa Suleiman na Suleiman ni Nabii wa Mwenyezi Mungu na daima jina lake linanasibishwa na busara na hekima. Shaaban Robert hakupungukiwa na bidhaa hizi mbili ambazo ni adimu katika ulimwengu wa leo. Mama mzazi wa Shaaban Robert naye alikuwa na jina zuri. Huyu aliitwa Mwanamwema.

Labda tutaisaidia jamii yetu tukijifunza kutoka katika historia ya maisha ya Shaaban Robert kwamba kuna umuhimu wa kuwapa watoto majina yaliyo mazuri. Na siyo kushikwa ghadhabu na kutoa majina ya kebehi, masimango na yenye kudumisha uhasama katika jamii. Tabia ya jirani kutoa jina ili kumkomoa yule waliyegombana naye si jambo linalosaidia sana jamii. Bali hudumisha uhasama na kujenga chuki vitu ambavyo ni hatari katika maendeleo ya jamii. Majina ya Shaaban bila shaka yana ujumbe mzuri ili nasi tuige, lakini tusitumbukie katika hatari ya kufanya ushirikina wa aina yoyote.

Bustani ya Washairi

Mwezi wa nane juani. Atapopenda Manani watakutana mjini wale wanaothamini lugha yetu ya maana. Lugha yetu ya thamani Kiswahili. Kando ya ziwa la maji Tanzania kuna mji unaoitwa Bukoba. Katika mji huo wapenzi wa Kiswahili watakutana ili kukumbuka miaka 50 ya kutawafu simba wa Uswahilini, mzoefu wa kufutu hoja, bilhususi ukishitadi utesi, Shaabani wa Robert. Na Malenga Al-Ustadhi Khamisi Sultani Wamwera mwana wa Lusende Nyipala yatetemeka yake jasadi, kwani mpaka wa leo hatuoneshi dalili ya kuenzi Kiswahili. Lakini kwake hakuna lugha yoyote nyingine yenye thamani kama ilivyo lugha yake ya Kiswahili. Na hino ndio lugha aliyoienzi Shaaban wa Robert. Wamwera anaimba:

LUGHA YANGU KISWAHILI

1 Bismillahi awali, Ndiwe Wewe Mhifadhi
Nipe nguvu ya akili, niseze yanayokidhi
Uyafanye yawe mali, yeyote yasimuudhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

2 Nakushukuru Jalali, kwa Lugha kunikabidhi
Lugha hii Kiswahili, yenye ladha bila ludhi
Kuisema, kunakili, kwangu naona faradhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

3 Nakipenda Kiswahili, kwa utamu wa lafidhi
Kwa kweli nakikubali, na moyoni nakiridhi
Lugha faswaha kubuli, wala haina gharadhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

4 Nakipenda kweli kweli, sithubutu kubughudhi
Yangu na ni ya asili, na sasa naihifadhi
Titi la mamiye mwali, linginewe halikidhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

5 Linginewe uaili, na kwangu lina ghamidhi
Kwenye lisani hudhili, huniletea maudhi
Hujiuliza maswali, mwenyewe nikawa kadhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

6 Nitasema Kiswahili, sitakiweka baadhi
Lugha yangu naijali, siweki utaaradhi
Naiomba Serikali, na waiwekee hadhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

7 Isemwe kila mahali, katika hii aridhi
Izungumzwe skuli, mahakama kwa Makadhi
Na waketipo manguli, wa bara letu mafadhi
Kwani isipate hadhi, Lugha yangu Kiswahili?

Al-Ustadh Khamisi S.S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu
Dar es Salaam

Beti amezicharanga Hamisi mwana wa Mbanga anawaasa wakembe; Jama punguza sarange. Kiswahili cha Malenga kimeachwa. Tulicho nacho sasa kimejaa mavumbi na mchanga. Hivyo lazima tutangaze kitali dhidi ya wenye fujo za kitatange. Wenye akili mawenge. Hao tuwavishe vilemba vyenye madoa ya kenge na waache kupiga kelele mfano wa kiberenge. Tokezeni Malenga lugha kuipa nusura. Kungwi anaimba;

LUGHA WANAIBANANGA

1 Nisikizeni mliko, enyi wajuzi wa kunga
Kamwe sivunji miiko, kuna linalonisonga
Na sileti chokochoko, ila kero zimezinga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

2 Langu kubwa sikitiko, yameachwa ya wahenga
Lugha yenye sisimko, Kiswahili cha malenga
Imetiwa sokomoko, kwa mavumbi na mchanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

3 Ni hawa mafundi koko, wasiojua kutunga
Ambao hupenda heko, na nishani kwa kuhonga
Wameleta machafuko, lugha inatangatanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

4 Masikini wa miweko, si mahiri wa kupanga
Tungo zao ni vituko, urari unawatinga
Hawapati suluhiko, kiburi kimewaenga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

5 Ni watu wa malimbuko, walolemewa ujinga
Si waja ni mbwa koko, kuwasamehe si kinga
Heri hata kwa viboko, tuanze kuwachabanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

6 Semi zao za mizuko, maghani zinavuruga
Hata wapi zitokako, hawaelezi kinaga
Vipi tukae kitako, tuchelee kuwaswaga?
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

7 Lugha yetu nyumbuliko, hawa wanaiboronga
Lahaja ziso na soko, wamezitwalia nanga
Hawatufai kuliko, wanatutia majanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

8 Sijui wapi mliko, manju wajua kihenga
Muje tuwashike shiko, hata wakome kuringa
Tuwarudi waendako, watazidisha vilanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

9 Nijulishe ukaako, Wamwera mwenye mianga
Kamata khanjari yako, na tuanze kujipanga
Tuwatimbe kwa mikoko, tukomeshe zao ngenga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

10 Shamte mwenye upako, wa ala za mitulinga
Wewe fundi milipuko, hebu chakata mzinga
Tufyeke hawa wanoko, fani wanaotobanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

11 Wamamba acha chereko, tumezingirwa visanga
Pasipo mchango wako, vigumu kuwakaanga
Hebu beba kita chako, na tuanze kuwalenga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

12 Gwiji mwenye lugha yako, Amiri wa Andanenga
Njoo tuzime kicheko, chao hawa mandundunga
Vunja unyamavu wako, tuwatie titimanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

13 Mazongera ungaliko, japo mandevu kaaga
Ukidekeza mchoko, lugha nayo itaaga
Njoo na sindano zako, tutibu zao mbalanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

14 Nafupisha maandiko, kwa hoja niliyojenga
Naomba lenu itiko, fani tuje kuikinga
Chonde hima tikisiko, lugha wanaichaanga
Fani wanaibananga, wasiojua mizungu

Abdullah Hamisi Mbanga (Kungwi)
Tambani - Mkurungana Pwani

Wakati huu tunapomkumbuka Shaaban Robert hakuna swali linaloweza kuwa zuri kuliko 'Hivi ushairi ni nini? Swali la kale je Shairi ni vina, mizani, muwala, Shairi ni nini? Uko wapi Bin Ame kijana mtoka Pemba? Wa Lusende jitokeze Mwalimu wetu Wamwera. Kungwi mpe mwana sharubati. Jiji kasoro bahari mwana wa Mikila tafadhali kula hali tupe nasisi tufaidi. Bundara wa Tabora mtunzi mwenye busara tafadhali tupe beti. Amiri mwana wa Sudi na beti nitakuletea. Ramadhani wa Shamte vipi kwenye bustani? Siku zino sikuoni! Nani aliyekuudhi? Swali la Ismaili Lisinge jibu lake twalitaka. Saidi bin Manoro ondoa penye kasoro;-

1 Bismillahi naanza, kwa jina lake Manani
Ni sifa zake muweza, Muumbaji kila fani
Mwenye kutupa mwangaza, Tumshukuru Manani
Au kupata dhumuni, niache kubunibuni

2 Sasa sauti napaza, natoa swali moyoni
Leo nami nauliza, washairi nijibuni
Na kama nikiwakwaza, basi nivumilieni
Au kupata dhumuni, niache kubunibuni

3 Mwenzenu nipo gizani, sijui vitu vya ndani
Nisije fika mwakani, nasina kitu kichwani
Shairi ni kitu gani, ni vina au mizani?
Hivi shairi ni nini, kutunga au kughani?

4 Nisomapo gazetini, moyo mno hutamani
Nami nije shika peni, lakini chanzo ni nini?
Wamamba nipe kiini, na mimi niwe kundini
Hivi shairi ni nini, kutunga au kughani?

5 Hivi shairi ni nini, beti zake au tuni?
Ame usiniacheni, nipe neno la yakini
Au ni vina vya nini, vyatakiwa m tamboni?
Hivi shairi ni nini, kutunga au kughani?

6 Wamwera upo kundini, unijibu kwa makini
Nipe elimu ya ndani, nami niwe furahani
Ili nipate dhumuni, niache kubunibuni
Hivi shairi ni nini, kutunga au kughani?

7 Siyo kwamba nakukera, Pazi mwana Mazongera
Nataka yako fikira, Mola Akupe ujira
Au ndio nyimbo bora, zampendeza baswira
Au kupata dhumuni, niache kubunibuni

8 Hapa ninaacha peni, majibu yangu nipeni
Nitapata ahuweni, nikisoma gazetini
Mola Alichowapeni, nami nipunguzieni
Au kupata dhumuni, niache kubunibuni

Ismaili Lisinge

Haya Wajuzi wa Kunga! Suguru Dume, baada ya kuchungulia sana humu kiungani kaona ni vyema aingie uwanjani, uwanja wa Bustani ya Mapenzi ya Mungu! Beti zake kwenye mashairi mawili hapa chini, hazioneshi kwamba yu Suguru bali yu Kilima, basi mkaribisheni.

BAHATI HAIWI MBAYA

1 Mungaketi utangani, wahadhirina mukawa
Nisikizani Hassani, leo kunga n'nagawa
Kaani mtamakani, musiwe na kupagawa
Bahati ni kitu chema, na katu haiwi mbaya

2 Ikinenwa mitaani, kule Mwanza na Dakawa
Kuibadili maani, ni sudi mbaya ikawa
Munaiweka rehani, itumiwavyo si sawa
Bahati ni kitu chema, na katu haiwi mbaya

3 Nuhusi litambuwani, ni tamshi maridhawa
Kwa hiyo badilikani, muwezoea ingawa
Lugha ipate uzani, na hadhi yake kujawa
Bahati ni kitu chema, na katu haiwi mbaya

4 Tuwate usakarani, nawanasihi wenzawa
Tujitoe lawamani, waja wapate chachawa
Tukabaki maishani, wazungupule tukawa
Bahati ni kitu chema, na katu haiwi mbaya

5 Nitamile nudhumani, hazikunja zangu mbawa
Kwa mli Bara na Pwani, ja wanan'ti wazawa
Niombae zindukani, msififize vipawa
Bahati ni kitu chema, na katu haiwi mbaya

Hassan Salum Deu (Suguru - Dume)
Simu:0715950585
Dar es salaam - Tanzania.

KUTOKOZA MALEMELE

1 Ni utomi wa nakama, kwa yangu mato mbonele
Utatoni ukazama, pasi kufikiri mbele
Uje upate nadama, ukutoke ukelele
Kutokoza malemele, ni utomi wa nakama

2 Vyema kuwata hasama, kuwa mtuvu nyemele
Siwe mtendi zahama, na majigambo utele
Wendo ukawasakama, kisa ukwasi belele
Kutokoza malemele, ni utomi wa nakama

3 Yuwa hishima gharama, wala usiwe chechele
Ola wakongi wa zama, tunguza wako wa vyele
Usije kushika tama, ukabakia chegele
Kutokoza malemele, ni utomi wa nakama

4 Utamakani azama, ja usikivu uwele
Kwetu waweza tazama, tu barobaro tuwele
Tukichelea lawama, kutokoza malemele
Kutokoza malemele, ni utomi wa nakama

5 Ni utamo naegama, kishaye nchechemele
Ela si mwene kuhama, nudhuma zijazo tele
Singapenda mukakwama, muna kunga muhemele
Kutokoza malemele, ni utomi wa nakama

Hassan Salum Deu (Suguru - Dume)
Simu:0715950585
Dar es salaam - Tanzania.

Ni nusu karne sasa toka Shabaan Robert atutoke. Ukiachilia mbali shule ya Sekondari iliyoko jijini Dar es salaam, taifa hili haliwezi kuonesha alama yoyote nyingine ya kumkumbuka mlezi huyu wa Kiswahili. Ustadh Khamisi Sultani Wamwera anatuomba wakati tunakumbuka miaka 50 ya toka afariki tuweke kumbukumbu ya kumheshimu mlezi huyu wa Kiswahili.

AKUMBUKWE SHAABAN MLEZI WA KISWAHILI

1. Ashukuruwe Jalali, Mwenyezi Mola Manani
Aliletalo kwa kweli, liwe kubwa au duni
Lazima tulikubali, hakuna cha upinzani
AKumbukwe Shaaban, Mlezi wa Kiswahili

2. Ni miaka hamsini, tangu Shaaban wa Roberti
Atoweke duniani, kwenda zendako nyimati
Twamuombea huweni, aingizwe fijanati
AKumbukwe Shaaban, Mlezi wa Kiswahili

3. Shaaban bin Robert, ali mtunzi mahiri
Muandishi hasanati, wa insha na mashairi
Kwayo ali madhubuti, hakuondokwa na ari
AKumbukwe Shaaban, Mlezi wa Kiswahili

4. Anajua kila mtu, na khasa uswahilini
Shaaban bingwa wetu, alijulika nchini
Kiswahili ndugu yetu, alijua si utani
AKumbukwe Shaaban, Mlezi wa Kiswahili

5. Alikielewa vyema, kalamu yake fususi
Akiandika huzama, kwenye kilindi cha rasi
Hakutaswa na kalima, maneno hayapapasi
AKumbukwe Shaaban, Mlezi wa Kiswahili

6. Alikuwa ni kurunzi, miale mikali sana
Akiangaza utunzi, lugha bila kutafuna

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

Kwa mashairi na tenzi, ni nani wa kufanana?
AKumbukwe Shaaban, Mlezi wa Kiswahili

Bila kuweka chumvi mji wa Bukoba kwa kiwango kikubwa cha kutia sururi, umejishughulisha kwa mapana na marefu kuenzi, kulinda, na kustawisha lugha ya Kiswahili. Mwalimu Kiimbila licha ya kuambiwa lugha kuvungavunga hebu punguza sarange, alifanya kazi adhimu ya kuamsha hamasa miongoni mwa wanafunzi wake pale Nyakato. Mara mbili Bukoba imebeba dhima ya mikutano ya UKUTA. Dodoma nayo kwa Kiswahili ni ngome madhubuti. Aliyekuwa Mwenyekiti wa UKUTA Marehemu Sihiyana Swalehe Mandevu Mtendamema anaomboleza kwa kutawafu watetezi wa Kiswahili. Anaomboleza;-

1 Habari tumezipata, kutoka kwa mashabiki
Si njema zina utata, nyonyo zimetaharuki
Mwenyekiti wa UKUTA, Kagera amefariki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

2 Waweke pema watunzi, Tunakuomba Maliki
Wakale na zile enzi, huko wasipate dhiki
Wametuachia majonzi, tunapika haviliki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

3 Wenzao hatuna raha, tutako hatufiki
Tumepoteza silaha, zile tukitamalaki
Limetupata jeraha, kokote halitibiki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

4 Kimetupata kihoro, umwitae haitiki
UKUTA una kasoro, doa halipangushiki
Kifo cha Bwana Zahoro, imepasuka bunduki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

5 Alikuwa mwanachama, shupavu hatingishiki
Hakuchelea gharama, tangu moja hadi laki
UKUTA ulisimama, katu hautetereki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

6 Kuna hilo na la pili, kubwa halisahauliki
Mtunzi wetu Jamili, ukivamia hutoki
Kufa bwana Jitukali, umevunjika mkuki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

7 Poleni Nywena Bukoba, na Dodoma marafiki
Ongezeko la misiba, siku zino kila wiki
Hayo tumwachie Toba, hakuna kitachobaki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

8 Naiweka kaditama, hali moyo hautaki
Nikizidi kulalama, hiyo katu siyo haki
Kwani kifo ni lazima, leo kile kesho hiki
Yailahi Yamaliki waweke pema watunzi

Kwa ajili ya Wahandisi kutafakari! Hizi hapa beti mbili za Mhandisi mwenzao. Shaaban Robert alitoa mwito tufanye tafakuri katika tungo.

WALA SI MAUZAUZA

1. Bismillah naanza, kubainisha kikinza
Hakitaki muangaza, ni kikinza penye kiza,
Mwangaza ukikijaza, ukinzani unaanza
Wala si mauzauza, Amejaalia Muweza

2. Pili naweka bayana, chaji hujamiiana
Chaji zinazofanana, huwa zinafukuzana
Zikitofautiana, ni kama bibi na bwana
Wala si mauzauza, Amejaalia Muweza

***Abedi, Amiri K. (Msafiri),* Dar es Salaam**

Watoto msibaki nyuma, chongeni penseli zenu, babu yenu, Mhariri wa Mapenzi ya Mungu ninakuhakikishieni sitokuwekeni kapuni, Inshallah. Na Shaaban Robert alisisitiza malezi ya watoto na moja katika tungo zake anasema '***mkunje samaki angali mbichi***'. Na shairi hili hapa chini linatupa matumaini.

ISLAM

1 Islamu ndiyo nura, iangazayo dunia
Islamu ni nusura, pale utapojifia
Lakini ukikufura, adhabu tajipatia
Islamu muongozo, ifate utaongoka

2 Islamu yafundisha, kusali hata kufunga
Islamu yakwepesha, yale mawi na majanga
Islamu yakingisha, maisha kuyatobanga
Islamu uongofu, fateni mtaongoka

3 Islamu yakataza, kulewa na kuongopa
Islamu yatufunza, Mwenyezi kumuogopa
Islamu yahimiza, yalo hovyo kuyaepa
Islamu uongofu, fateni mtaongoka

Sir Zafrullah A. Ame
(darasa la tano)
Safina - Temeke, Dar es Salaam

Mistari ya Johari ya Sheikh Shaaban Suleiman Ufukwe (Al-Maaruf Shaaban Robert)

Na Mwandishi wetu

Waandishi wamepewa hidaya ya kufinyanga lugha nayo ikafinyangika vilivyo. Katika ufinyanzi huo panatokea mistari ya johari ambayo imebeba ujumbe mzito. Kwa uzuri wa maelezo ulioambatana na ufupi wa maneno yenyewe inakuwa rahisi kunukuu mawazo hayo na yakakusaidia kusema uliyokuwa unataka kusema. Itakuwa ni siku yangu ya fahari nikisikia katika mikutano mikubwa hata midogo kiongozi wangu au mwakilishi wa taifa langu akimnukuu mmoja wa waandishi wetu kama vile Muingereza anavyoona fahari kumnukuu William Shakespear, Mrusi Tolstoy, India - Tagore, Ujerumani - Goethe, Ufaransa - Victor Hugo, Pakistan - Iqbal, Nigeria - Chinua Achebe, orodha ni ndefu. Tunatoa ushahidi wa kuonesha ya kwamba yapo ya kunukuu kutoka kwenye kalamu ya Shaabani Robert.

"... Kipawa chochote cha mtu kama hakikuongozwa vyema huweza kuwa hatari au maangamizi kwa wengine ..." (Kusadikika Uk.1)

"... mchwa ukikaribia kuangamizwa hufanywa kumbikumbi na huoteshwa mabawa mawili..." (Kusadikika Uk.4)

"... kama watu waliokusudiwa kuwa mwenge kwa wengine wangalikuwa wakingojea shangwe la watu kabla ya kuanzisha makusudi yao maendeleo katika maisha yangaliadimika ..." (Kusadikika Uk.7)

" ... siwezi kuikana kweli kwa kuchelea upweke wa kitambo, nikajinyima ushirika wa milele unaotazamiwa kutokea baada ya kushindwa kwa uongo ..." (Kusadikika Uk.9)

"... Kwa desturi, maisha huwaficha watu wake bora mpaka tokeo kubwa litokee ... " (Kusadikika Uk.12)

"... Haja isiyoridhishwa husumbua fikira kama kiu isiyozimwa isumbuavyo koo siku zote ..." (Kusadikika Uk.16)

"... Inastaajabisha kwa nini dunia haitumii akili nyingi kwa kuijenga amani ya daima badala ya kuitumia nguvu nyingi kwa kuitafuta amani ya kitambo tu ..." (Kusadikika Uk.19)
"...Watu waliishi duniani kwa matendo yao, sio kwa sura zao ..." (Wasifu wa Siti binti Saad uk.25)
"...tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno, haja ikishughulikiwa kwa matendo hupaikana upesi, lakini ikishughulikiwa kwa maneno huchelewa kama sadaka ..." (Adili na nduguze uk.2)

"... kula uhondo kwataka matendo, asiye matendo hula uvundo ..." (Adili na nduguze uk.22)

" ... Litakalo rai mbili kwa moja haliwi jema ... " (Insha na Mashairi uk.75)

"... Wino wa wanachuoni thamaniye maradufu,
Huongoza duniani, watu kuwa watukufu" ... (Insha na Mashairi uk.11)

"...Kila lugha ni johari, shika vema kweli hiyo
Mkosa lugha fakiri, weka katika sikio" ... (Insha na Mashairi uk.13)
"Chuki uchafu wa moyo
Ni hasara kuwa nayo
Walio na mausio
Huikana kuwa mwenzi" (Mapenzi bora uk.10)

Sheikh Shaaban Suleiman Ufukwe,
(Al-Maaruf Shaaban Robert)

UJUMBE KUTOKA KWA MHARIRI WA MAPENZI YA MUNGU

Bodi ya Mapenzi ya Mungu inafarijika na wale wote wanaotuandikia kutupa pongezi kwa hicho kidogo tunachokitoa na wale wanaotusahihisha mahali wanapofikiri ya kwamba tumekosea. Tunawashukuru sana na kwa hakika wanatimiza wajibu wao. Gazeti ni watu na watu wenyewe ndiyo nyinyi. Si rahisi kutaja majina yote, lakini Bwana Simbila wa Tabora tunapata barua zake za kututia moyo tunamshukuru sana. Wale wanaoona kasoro nao tunawashukuru, ushauri wao tunauzingatia na kuuheshimu. Upungufu wowote unaojitokeza ni ule ule upungufu wa kibinadamu na hivyo tuendelee kuombeana ili sote kwa pamoja tuweze kutimiza wajibu wa kumfikishia binadamu ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as).

Mkutano wa amani Ikwiriri ulikuwa wa mafanikio

Na Mwalimu Nassor Hussein
Kisusa – Ikwiriri Rufiji.

Jumuiva ya Waislam wa Ahmadiva Jamati za Kibiti na Ikwiriri zilifanikiwa kuandaa Mkutano wa Amani. Mkutano huo ulifanvika tarehe 15 June 2013 katika ukumbi wa Chuo cha Maendeleo (FDC) Ikwiriri. Wageni toka kada mbali mbali walihudhufia katika mkutano huo. Miongoni mwa wageni hao, alikuwepo Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Mheshimiwa Nurdini Babu, Mkurugenzi Mtendaji (W) Afisa Usalama wa Taifa (W) O.C.D, Kaimu Mkurugenzi (W) na Mwenyekiti wa Halmashauri (W). Mgeni rasmi katika mkutano huo alikuwa ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Mheshimiwa Nurdin Babu.



Rais wa Mkoa wa Pwani Bw. Yusuf Shaaban Malinda akiwakaribisha wageni kwenye mkutano wa siku ya amani Ikwiriri. Kushotoni mwake ni Mkuu wa Wilaya ya Rufiji Mheshimiwa Nurdini Babu

Kama kawaida, Jamaat iliwakilisha mada kuu mbili sawa na makusudio ya mkutano. Mada ya kwanza ilitolewa na mwl. Abdallah Khamisi Mbanga. Pamoja na mambo mengine, pia alieleza historia ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiya hapa nchini. Alieleza ya kwamba tangu Jumuiya ianzishwe hapa nchini, imekuwa ikijishughulisha zaidi katika kuelimisha na kufundisha mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islamu. Lakini pia jumuiya ikiwa ni sehemu ya jamii, haikuwa nyuma katika kuwatumikia wananchi katika taifa hili. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, katika jumuiya tunalo shirika la ***Humanity First*** (Ubinadamu kwanza). Shirika hili limeweza kutoa huduma mbali mbali katika mikoa tofauti, ikiwemo ukarabati wa visima vya maji safi, ujenzi wa vituo vya afya na ujenzi wa shule za msingi na sekondari.

Kuhusu swala zima la amani, mwl. alieleza ya kwamba, tangu jumuiya iliposajiliwa hapa nchini, takribani miaka sabini sasa, haijawahi kupanga wala kushiriki katika vurugu zozote, ziwe ni za kidini au za kisiasa. Akasisitiza kwamba, maandamano yanayoambatana na uvunjaji wa amani, kwa kuharibu, mali za serikali na raia, japokuwa vitendo hivyo vinaweza kufanywa na vikundi fulani kwa mgongo wa uislamu, ukweli utabaki pale pale ya kwamba mambo hayo siyo katika mafundisho ya dini tukufu ya Islam, abadani.

Katika maandiko matakatifu, ndani ya Qur'an tukufu, Mwenyezi Mungu amekataza kutumia mabavu kwa kuwalazimisha wengine kuwaingiza katika dini.
(Qur. 2:251). Na kama kuna watu wanaofanya mambo hayo, basi hufanya hivyo kwa maslahi binafsi.

Mwalimu alimalizia hotuba yake kwa kusema ya kwamba, siku zote kauli mbiu yetu katika Jumuiya ni hii tu, ya kwamba UPENDO KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE.

Naye Maulana Alhaji Sheikh Bakri Abedi Kaluta, ambaye ni mwenyekiti wa Dawati la Kiswahili katika Ahmadiya tawi la Tanzania, mkoani Morogoro, alikuwa miongoni mwa watoa mada. Msingi wa mada yake aliujenga toka ndani ya Qur'an tukufu, katika (Sura 2:31) Inayosema:- Na kumbuka Mola wako alipowaambia malaika mimi nitamuweka Khalifa katika ardhi Akifafanua aya hii, Maulana Kaluta alisema tangu zama, za nabii Adamu (as) mpaka hivi leo, Mwenyezi Mungu ameendelea kutuma Makhalifa wake katika ardhi sawa na haja ya wakati, ili kuwafanya wanadamu wamwepuke yule mfalme wa giza (Ibilisi) na waingie katika ufalme wa Mungu. Lakini kwa bahati mbaya kila mara Mwenyezi Mungu anapotuma manabii, hujitokeza makundi mawili. Kundi moja la wachache humpokea Nabii huku wakishangilia utukufu wa Mungu unaoambatana na uokovu, unaopatikana kupitia Nabii wa zama. lIihali kundi jingine hujitenga mbali na utaratibu huo wa kimbingu. Katika nyakati hizo, wakuu wa dini, hufikiri kwamba nabii aliyetumwa, pengine amekuja kuwanyang'anya ukubwa. Hivyo huwafanya wafuasi wao, kujenga chuki dhidi ya nabii wa Mwenyezi Mungu, pamoja na wafuasi wake. Ni kipindi hiki ambacho wale waliochagua kufungamana na nabii wa zama, huanza kunyanyaswa kwa kunyimwa haki zao za msingi, kukejeliwa, kutukanwa, na hata kuuawa. Haya huwa ni mambo ya kawaida katika nyakati hizo.

Akifafanua kuhusu vita aliyopigana Mtume s.a.w. Alhaji Bakri alisema kwamba vita vile vilikuwa vya kulazimishwa. Mtume s.a.w. hakuwa na matakwa ya kuanzisha vita hiyo. Kwani kwa muda huo wote tangu Mtume s.a.w. alipoutangazia ulimwengu ya kwamba yeye ni nabii na Mtume wa Mwenyezi Mungu, roho ya Ibilisi yule yule aliyejiinua kwa kufanya kiburi kwa kutokumtii Adamu, kama alivyohukumiwa na Mwenyezi Mungu, ni roho hiyo hiyo iliyojiinua kwa mara nyingine zama za Mtume mtukufu s.a.w. akiwachochea watu kufanya ghasia na mauaji dhidi ya Nabii wa Mwenyezi Mungu na wafuasi wake.
Katika kipindi hicho kigumu, hawakuwa na njia isipokuwa kukimbia nchi yao. Wakawa wakimbizi kwenye nchi za kigeni. Mtume s.a.w. pamoja na ndugu wa imani walihama kuelekea Madina, ilihali kundi jingine, bila kutegemea walijikuta kwenye ardhi ya Afrika Mashariki katika nchi ya Ethiopia. Kwa uchache, Maulana Sahib aliwataja baadhi yao waliokuwemo kwenye msafara huo. Wa kwanza ni Hadhrat Uthmani Bin Affan (ra) na mkewe Bi Ruqayya Binti Rasuli s.a.w. Abdurhman Bin Auf, Zuberi Bin AI-Awwam, na Mus'ab Bin Umair, kwa kutaja wachache.
Sheikh Bakri akaeleza ya kwamba, Ikumbukwe ya kuwa mfalme wa Ethiopia katika siku hizo, alijulikana kwa jina la Nagus Mkristo. Ijapokuwa alikuwa mfuasi wa dini hiyo ya kikristo, alihakikisha ya kwamba wageni wake ambao walikuwa ni waislam wanaishi maisha ya amani katika ufalme wake.
Aliwatendea vema sawa na ubinadamu. Hata walipotumwa wajumbe wa maadui kutoka Maka ili kumrubuni mfalme Nagus ili wafukuzwe waislam, mfalme alikataa. Wajumbe wale wakarejea Maka vichwa chini kwa kuelemewa na aibu.
Haya yalikuwa ni matokeo yaliyoletwa na mfalme muadilifu mkristo.
Hapa Sheikh Bakri akasisitiza ya kwamba, tofauti za dini au madhehebu isiwe ni sababu ya kuleta mafarakano na utengano katika jamii, kwa sababu mambo hayo yakiachiwa hupelekea uvunjifu wa amani katika taifa. Kilicho kikubwa na cha msingi zaidi, ni kuheshimiana, kupendana, na kusaidiana katika nyakati za matatizo, kama alivyofanya mfalme Nagus kwa Waislam.

Naye kwa upande wake Mheshimiwa mkuu wa wilaya ya Rufiji Bw. Nurdini Babu, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mkutano huo, alisema kwamba amefarijika sana na kuridhishwa mno, kwa jinsi Jamaat Ahmadiyya inavyopanga, kuratibu na kusimamia majukumu yake. Mnaposema nyinyi ni jumuiya, ina maana kwamba ninyi mnazo kanuni na taratibu zenu zinazo kuongozeni, ndiyo maana mnaweza kufanya haya yote mliyoyaeleza hapa. Mnachimba visima vya maji, mnajenga shule, mnajenga hospitali. Hizi zote bila shaka ni huduma za jamii. Mtu wa dini yoyote au dhehebu lolote yuko huru kuitumia, alisema Mheshimiwa Babu. Pia katika hotuba yake alieleza ya kwamba siku hizi wapo baadhi ya watu wachache wanaojaribu kuvuruga amani ya nchi, kwa kuleta udini, siasa za chuki na ukabila. Akawataka wananchi wote kuwa macho dhidi ya watu wa namna hiyo, kwani hao hawaitakii mema nchi yetu. Tuendelee kuilinda na kuienzi amani iliyopo nchini. Kwani amani ikitoweka hata mikutano ya namna hii haitafanyika.
Akaeleza ya kwamba Jumuiya ya Ahmadiya imeonyesha njia kwa kuandaa mkutano kama huu. Kwa hiyo na sisi kama serikali tutaandaa mkutano siku zijazo. Tutaandaa mkutano ambao utashirikisha viongozi wa dini zote, ili tuweze kuona jinsi ya kuimarisha amani katika wilaya ya Rufiji na taifa kwa ujumla. Katika mkutano huo tutakaoandaa, watoa mada waliohutubu leo, Sheikh Bakri na Sheikh Abdallah, tutawaita siku hiyo ili waje wayaseme yale yale waliyoyasema leo ili na wenzenu wapate kujifunza kutoka kwenu. Akasema nimefurahishwa kwa kuona ufasaha katika kujieleza kwenu. Ni siku hiyo ambapo mheshimiwa mkuu wa wilaya alizindua kauli mbiu ya amani wilaya ya Rufiji. Kauli mbiu ina maneno haya:-

Amani Rufiji - Rufiji amani.

Kabla ya kufika mwisho wa makala haya, niwashukuru ndugu wafuatao walioshiriki kuratibu na kufanikisha kuandaa mkutano huu:-
(1) Amir Jamaat Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry aliyeidhinisha gharama zote za mkutano.
(2) Majlisi Amila Tawi la Kibiti, ikiongozwa na Rais wa mkoa Bw. Yusufu S. Malinda na kaimu Mbashiri wa mkoa mwl. Yusufu M. Mbawala, kwa ufuatiliaji na ushauri.
(3) Majlisi Amila tawi la Ikwiriri, ikiongozwa na Rais wa tawi Bw. Munir S. Mnungu na katibu wa tawi Bw. Haji H. Mbanga kwa kusambaza barua za mwaliko kwa watu mbalimbali.
Mwenyezi Awabariki wote na kuwalipa kwa juhudi yao. Amin.

Eid Mubarak

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry pamoja na Wajumbe wote wa Bodi ya Uhariri wa Gazeti lenu la Mapenzi ya Mungu wanapenda kuwatakia Waislamu wote na wasomaji wa Gazeti la Mapenzi ya Mungu

Eid Mubarak

JALSA SALANA 2013

Wanajumuiya wote wanaarifiwa kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika kwenye siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 27, 28 na 29 Septemba 2013, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah.

Wanajumuiya wote wanahimizwa kuhudhuria Jalsa hiyo.

Vijana tuuhalisishe Uislamu wetu, kuepuka ya Pappiss Demba Cisse wa New castle Unt.

Na Ayoub Mtekateka,
Dar es Salaam

Hivi karibuni ulimwengu wa wapenda michezo hasa ule wa kandanda ulikumbwa na habari iliyowashtua wengi miongoni mwa wadau wake. Habari hiyo iliyopamba kurasa kadhaa za michezo za magazeti mbalimbali ya hapa nchini kwetu na duniani kote zilikuwa zinaulenga mchezo wenye kupendwa na wengi Duniani, kabumbu. Wengi wa walioguswa na habari hiyo ya kishujaa walikuwa ni waumini wa dini ya Islam ulimwenguni kote hasa wanamichezo.

Habari hizo zilikuwa zinamhusu mchezaji wa kimagharibi anayekipiga katika klabu ya Newcastle United yenye makao yake mjini Newcastle nchini Uingereza. Namzungumzia mchezaji Papiss Demba Cisse muislamu aliyezaliwa nchini Senegal Juni 3, 1985. Mchezaji huyo aliyechukuliwa kama shujaa miongoni mwa wafuasi wa dini ya Islam kwa kitendo chake cha kukataa kuvaa jezi za klabu yake zilizo na nembo ya mdhamini wa klabu hiyo kampuni inayojihusisha na kuchezesha kamari ya WONGA.

Binafsi, nimewahi kununua nakala kadhaa za magazeti yaliyokuwa na habari za mchezaji huyo japo mengi kati ya hayo hayakuwa na habari mpya zaidi ya kuirudia hiyo hiyo tu tena kwa namna tofauti. Si kawaida yangu kununua magazeti kwa staili niliyoitumia wakati nafuatilia habari hiyo iliyonisisimua kwa kiasi kikubwa. Jambo lililovuta hisia zangu ni kitendo cha kuona mwanasoka wa Kiislam tena kutoka nchi za magharibi mwa bara la Afrika ambapo wengi wetu tunatambua ya kwamba ni nchi zilizogubikwa na giza la starehe na maovu ya kila namna kama ilivyo kwa mataifa ya Ulaya akijitahidi kutetea imani yake katika ardhi ya Wazungu ambao Uislamu kwao ni Ugaidi. Pappiss, ilikuwa aingie kwenye orodha ya wanasoka wachache waislam kutoka magharibi ambao wamekuwa wakijitahidi kutetea mafundisho ya dini yao tukufu kupitia mchezo wa soka ambao wengi wa wachezaji walio na imani kama yeye ni nadra sana kukuta wakiwa na msimamo aliojaribu kutudanganya nao akina 'sisi'.

Wachezaji wenye imani ya kiislamu kutoka katika nchi za magharibi mara nyingi wamekuwa wakiripotiwa kuwa na msimamo mkali wa dini yao hasa pale inapotokea mtu asiye muislamu kuwaingilia katika mambo ya kiimani. Mifano michache ya wachezaji waliowahi kuwa na msimamo kuhusu dini yao na kukataa kuvaa jezi za klabu zao zenye nembo yenye kuhamasisha mchezo wa kamari kinyume na maadili na mafundisho ya kiislamu na wakafanikiwa. Frederic Umar Kanoute aliyezaliwa Septemba 2, 1977 nchini Mali, aliwahi kufanya hivyo wakati akiitumikia klabu yake ya Sevilla ya nchini Uhispania kuanzia msimu wa 2005/2012. Mchezaji huyo kwa sasa anaichezea klabu ya Beijing Guoijan ya nchini China. Mchezaji huyo anabaki katika historia ya wanamichezo wachache wa Kiafrika ambao walikuwa na msimamo wa dini ndani na nje ya uwanja na wakaheshimika



Pappss Demba Cisse akishangilia moja ya magoli aliyoifungia timu yake Newcastle United msimu uliopita. (Pichga: Na Ayoub Mtekateka kwa hisani ya Mtandao)

Jambo lililonifanya niandike habari hii nzito, si suala la ushujaa wa Pappiss Demba Cisse kukataa kuvaa jezi za klabu yake zenye kudhaminiwa na wacheza kamari, bali ni kitendo chake kisicho cha kidini na kiungawana alichokifanya siku chache baada ya kuushawishi umma wa kiislamu na wasio waislamu kuwa yeye ni muumini 'mwenye msimamo' na mwenye kufuata sheria za kiislamu ipasavyo.

Mchezaji huyo amekutwa akicheza kamari katika Cassino maarufu la nchini Uingereza lililopo katikati ya mji wa Newcastle jambo ambalo ni kinyume kabisa na mafundisho aliyodai kuyatetea. Mbaya zaidi kafanya hivyo ndani usiku wa mwezi huu wa Ramadhani ambapo waislamu duniani kote wapo katika kutimiza mojawapo ya nguzo muhimu za dini yao ya Kiislamu kwa kuacha kula, kunywa, na kila lililo katika uwezo wao ili kujiweka karibu na Mola wao na kuomba msamaha wa makosa yao. Kitendo hiki kinaushangaza ulimwengu na hata wafuasi wa dini hii tukufu ya Islamu ambao wanaamini kamari ni dhambi hatari ambayo inaeweza kuiangamiza jamii. Ndani ya Kurani Tukufu, kitabu ambacho ndicho mchezaji huyo alidai kufuata mafundisho yake ili kuficha 'ufedhuli wake', Mwenyezi Mungu anasema:

"Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema: Katika hivyo mna dhambi kuu na manufaa kwa watu pia, lakini dhambi yao ni kubwa kuliko manufaa yao….."

Kitendo hicho cha Papiss Demba Cisse kukutwa akicheza kamari katika Cassino hiyo kimezua mjadala mkubwa miongoni mwa wadau wa soka hususani mashabiki na viongozi wa klabu hiyo ambao wanahoji juu ya ukweli wa mchezaji huyo kufuata maadili ya kiislamu kutokana na kitendo chake hicho kinachoonekana kukiuka mafundisho ya kiislamu aliyodai kuyatetea. Wapo wanaoshangazwa zaidi na hili. Wengi wao ni wale waliokuwa wakiamini mchezaji huyo angesimamia vyema msimamo wake huo.
Cisse ambaye aliachwa na klabu yake katika ziara ya timu hiyo ya kujiandaa na msimu mpya wa ligi nchini Ureno, alikuwa katika mgogoro mkubwa na klabu yake na kutishia kuondoka baada ya klabu hiyo kupata mdhamini mpya, WONGA, kampuni inayojishughulisha na michezo ya kamari kwa kile alichodai 'anakiuka maadili ya kiislamu' kwa kuvaa jezi zenye nembo inayohamasisha kamari.
Nimeona ni vema nitumie sakata la mchezaji huyu 'muislamu' kuwatahadharisha khuddam wenzangu na waislam wengine kwa ujumla ya kwamba tujitahidi kuishi maisha yenye kumpendeza Mwenyezi Mungu kwa kuuhalisisha uislamu wetu kwa wengine. Tuyatende kwa ukweli wa moyo yale tunayoyahubiri. Tusiseme yale tusiyoyafanya, tutahukumiwa na watu na Mungu pia.

Wapo wengi wetu ambao haya yaliyofanywa na mchezaji huyu ni sehemu ya maisha yao ya kila siku huku upande wao wa pili wakijinasibisha na uislamu. Wengi wamekuwa wakiudanganya ulimwengu kuwa ni wafuasi wazuri wa uislamu huku matendo wanayoyafanya hayaendani kabisa na maneno yao. Wanatafuta kumdanganya Mwenyezi Mungu hali kwa Mwenyezi Mungu hakuna kinachofichikana.
Wapo khuddam wenye vipaji vingi ambavyo vinaweza kuwafikisha huko wanakocheza akina Pappiss Demba Cisse, wajifunze kupitia yeye ili uislamu wao usije ukaingia doa la unafiki. Wakati ndio huu wa wao kubadilika na kuwa na msimamo wa kweli wa dini yao wasisubiri jua lizame wakautia aibu uislamu kama alivyofanya mchezaji huyu kijana.
Tunapaswa kujiuliza; hivi ni kweli mtu huyu anastahili kuigwa na wanamichezo wengine wa kiislamu ambao walimchukulia kama mfano wao wa kuigwa katika suala zima la kuitetea misingi na taratibu za imani yao katika michezo? Je? Alichokifanya ni sehemu ya uislamu? Kama jibu la maswali haya mawili ni 'Hapana', basi tunapaswa kubadilika kuanzia sasa ili kuyaepuka yaliyomkuta mwenzetu huyu.

NB: Toleo lijalo inshallah tutawaletea baadhi ya wachezaji wa kiislamu na wenye majina makubwa ulimwenguni. Dua zenu njema ni muhimu kwetu. Nawatakia mfungo mwema wa Ramadhani pamoja Eid Mubarak!- Mwandishi

Mpenzi wa Kiswahili

Na Mchunguzi

Wapo watu Mwenyezi Mungu Amewajaalia upole unaoambatana na usemaji wa taratibu na anapotembea katika ardhi anakumbuka aya ile "Walaa tamshi fil ardhi malahaa" (Wala usitembee katika ardhi kwa maringo). Watu hawa aghalabu huwa na vitu vingi bali hawavitoi mpaka wamechokozwa au wameumia. Sifa zote hizo kazichuma Alhaji Abdallah Salim Seif Al-Habsy ambaye yeye hapendi hayo tuliyosema juu yake lakini sisi tunasisitiza ya kwamba kwa kiwango chochote utakachotumia yeye ni mtaalamu na mpenzi wa lugha ya Kiswahili.

Mapenzi aliyo nayo kwa lugha ya Kiswahili hayana mfano. Kwa muda mrefu amefanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili na tayari amekwishakusanya methali takriban 700 na amekusanya mashairi yake tayari yatolewe katika sura ya diwani.

Al-haji Abdallah alikuwa rafiki mkubwa wa Mshairi Mwinyi Hatibu Mohamedi mtunzi mahiri wa mashairi ya Kiswahili. Ukiwakuta wawili hao wanachambua mashairi na kuzungumzia juu ya baadhi ya maneno ya Kiswahili utakatisha safari yako. Alhaji pia alifahamiana vilivyo na Shaaban Robert, na Shaaban Robert alipofariki urafiki huo ukahamia kwa mwanae Iqbal ambaye amemtumia ubeti wa kumpongeza Alhaji kwa diwani yake. Iqbal anaimba;
Abdallah bin Seifu,



Alhaji Abdallah Salim Seif Al-Habsy

nakutumia pongezi
Kazi ulizosanifu,
hakika ndiwe mjuzi
Huna chembe hitilafu,
umefuzu yako kozi
Msingi wa kazi bora,
ni hiki kitabu chako.

Litakuwa jambo jema, nikuonjeshe angalau kwa akali uhondo uliyomo katika diwani yake.
Kesha ukijikalifu,
kwa kuuza usingizi
Faidaye maradufu,
kwa wanaomaizi
Muda wao husadifu,
wakapata ufumbuzi
Kwa kuuza usingizi,
kukesha kuna faida

Na ubeti mwingine anasema;
Iwe ndogo ja sindano,
tundu ya kiasi hicho
Umbali uso mfano,
kipande ukifuacho
Sitoumia yangu meno,
wala kupepesa jicho

Akieleza juu ya mtu ambaye hana shabaha yoyote katika maisha, na wala hajui aendako Alhaji Abdallah anasema ni muhali kwa mtu huyo kukadiriwa kufika, kwani hajui aendako. Alhaji anaimba;

Naanza langu shairi,
kumshukuru Rabbuka
Mwenye mwingi utajiri,
Mpweke Alotukuka
Kunako zote sayari,
katu hana mshirika
Asiyejua endako,
hakadiriwi kufika.

Kama wasemavyo Waswahili, 'Mgaagaa na upwa, hali wali mkavu'. Ukipitia diwani ya Al-Haji Abdallah Salim Seif Al-Habsy hutapata hasara yoyote, bali kuna faida tele. Licha ya kukuonya na kukupa tahadhari juu ya ghururi za dunia, bila shaka utaongeza msamiati wako. Kwa mathalani maneno yafuatayo; charana maana yake sumni, kiganuni maana yake hadithi, halasa maana yake hutuba ya nasaha, mlelema maana yake jembe, roli ya ng'ombe maana yake kundi la ng'ombe.

Wapenzi wa namna hii wa lugha ya Kiswahili wanatakiwa waheshimiwe na wapewe moyo ili kazi zao ziweze kusaidia maendeleo ya Kiswahili. Tabu yetu katika nchi hii ni kutoa sifa tele mtu akisha ondoka, lakini akiwepo hakuna anayemjali wala kumthamini. Nusu karne hii toka Shaaban Robert afariki itupe changamoto ya kusahau yaliyopita na tujenge upya mapenzi juu ya lugha yetu ya Kiswahili.

Unyenyekevu na Upole njia ya kumfikia Mungu

Kutoka uk. 12

mwaminio hana budi awe mpole, mnyenyekevu na asiye na majivuno. Manabii wa Mwenyezi Mungu ni wa pekee katika sifa hizi, wao wanao upole na unyenyekevu uliopita kiasi. Kuliko wengine, sifa hii aliionyesha zaidi Mtukufu Mtume s.a.w. Mmoja ya watumishi wake aliwahi kuulizwa ni vipi Mtukufu Mtume s.a.w. alikuwa anamfanyia. Akajibu ukweli ni kuwa Mtume alimtumikia yeye zaidi kuliko yeye alivyomtumikia Mtume s.a.w. Msalie Eee Allah Muhammad na ahali za Muhammad na umbariki na kumhifadhi. Yeye ni mfano ulio bora wa maadili na unyenyekevu. Ni kweli kwamba miongoni mwa jamaa za mtu wanaomtumikia zaidi ni wale wanaomzunguka muda wote. Hivyo kama mtu anataka kupima unyenyekvu, upole, uvumilivu na subira ya mtu basi wanaomzunguka mtu.

Huu ndio mfano wenye baraka ambao uma wa Kiislam umehimizwa kuufata. Wakati Qur'an tukufu inatuamuru kufuata amri za Mwenyezi Mungu, mfano ulio bora na ulio kamilika ni dhati ya Mtukufu Mtume s.a.w. Akielezea kiwango chake cha juu cha Uchamungu, Mwenyezi Mungu ana mwambia atangaze kwamba kuabudu kwake kote ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu na hana tamaa yoyote ya kibinafsi kupitia kumwabudu kwake Mwenyezi Mungu. Kima cha tanagzo hili: Qul Inna swalaty wanusuky wamahyaaya wamaamty lillahi Rabilialaamiin 'Sema hakika sala yangu na sadaka yangu na uzima wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mwumba wa ulimwengu..' (6:163) na hiki ni kiwango cha daraja la juu kabisa kiasi hiki kwamba zaidi ya Mtukufu Mtume s.a.w. hakuna anayeweza kukifikia kwa ukamilifu wake. Mwenyezi Mungu pia anasema kuhusiana na kusubiri na kuvumilia : Wamaa yulaqaahaa ila lladhiina swabaruu wamaa yulaqqahaa ilaa dhuu hadhi adhiim, 'Lakini hakuna apewaye hilo isipokuwa wale wenye kusimama imara na hakuna apewaye hilo isipokuwa yule mwenye hadhi kubwa.' (41:36)

Zama tuchunguzapo maisha ya Mtukufu Mtume s.a.w. tunagundua mifano ya kiwango cha hali ya juu kabisa cha uvumilivu na subira yake katika matatizo na mashaka ya kifamilia, matatizo na mashaka ya kimwili na matatizo na mashaka ya kijamii.

Humo mote alionyesha mifano ya hali ya juu ya tabia njema ya uvumilivu na kusubiri. Kule Taifa aliuokoa mji dhidi ya maangamizi pamoja na kwamba Mwenyezi Mungu mwenyewe alimpa hiari ya chaguo la kutokea kwa hilo. Ingawaje pamoja na maumivu makali aliyosababishiwa na watu wakorofi wa Taifa yeye alisema hapana, wasiangamizwe. Wakati Fulani wafuasi wake kwa kuchoshwa na mateso ya maadui zao walimuomba afanye dua ya kuangamizwa kundi Fulani la maadui lakini yeye akawaombea waongozwe na hivyo akawafunza wafuasi wake kuwa wavumilivu na kwamba njia iliyo bora ya kulipiza kisasi haikuwa kuwaombea waangamizwe bali kuwaombea waongozwe na kuonyesha kiwango cha juu cha subira na uvumilivu. Mifano ya uvumilivu wa mtukufu Mutme s.a.w. inaweza kuonekana katika kila hali ya maisha yake. Juu ya Hili Masihi Aliyeahidiwa amesema: Tumepatiwa mfano ulio bora na kamili kabisa kwa ajili ya kufikia ukaribu na Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ametuamuru kuuigiza na pia ametupa maelekezo kadha ambayo tukiyafuata tutafikia ukaribu Naye. Pamoja na maelekezo yote na mfano ulio bora kabisa bado Mwenyezi Mungu Ameelekeza kwamba ukaribu Naye unaweza tu kufikiwa iwapo mtu atakuwa mpole na mnyenyekevu.

Aya iliyosomwa mwanzoni inafafanu njia za kushika unyenyekevu na za kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu. Zinasema kwamba ukaribu na Mwenyezi Mungu unaweza tu kufikiwa iwapo mtu atafikia kiwango cha juu cha unyenyekevu. Kinyume na hilo mtu hawezi kamwe kukanyaga njia ya kufuata amri za Mwenyezi Mungu kwa ukweli iwapo hajautafuta msaada Wake kwa upole na unyenyekevu. Hivyo kila mmoja wetu ni lazima autafute msaada wa Mwenyezi Mungu kwa upole na unyenyekevu. Mafundisho ya Mwenyezi Mungu ndani ya Quran Tukufu yametolewa ama kwa amri za moja kwa moja au kwa kupitia simulizi za Manabii wa kabla. Kila kitu ndani ya Qurani tukufu ni nasaha kw awaaminio. Hivyo inaamriwa kushika unyenyekevu na kujitahidi kupata msaada wa Mwenyezi Mungu. Hadi pale roho ya 'Na ombeni msaada' itakapoeleweka haiwezekani mtu kuelewa na kushika njia za utawa. Na roho ya 'Na ombeni msaada' inazalika tu kutokana na unyenyekevu na upole na kwa kuelewa barabara kwamba sifa tu za mtu binafsi haziwezi kumfanya apate thamani ya kupata ukaribu na Mweneyzi Mungu waila ni rehema na msaada wa Mwenyezi Mungu pekee ndio unaweza kuyafanya maisha yetu na yajayo yawe na thamani.

Hivyo tumwombe Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na kujitupa kwake kwa hali ya juu: Eee Mola wetu kwa rehema na ukarimu wako Utujie na msaada wako na utufundishe njia za kukuridhisha Wewe na utufunze za kukuabudu Wewe na kiwango cha kusubiria kinachokuridhisha Wewe. Inasemwa kwamba iwapo unatafuta msaada wa Mwenyezi Mungu na Baraka Zake basi onyesha unyenyekevu na zidisha kiwango chako cha subira na uvumilivu. Makamusi yanalieleza neno Sabr kuwa ni neno la Kiarabu ambalo maana tafsiri yake ni subira ikimaanisha: kubeba maumivu kwa heshima bila ya kulalamika wala kupiga kelele, pia inaamnisha kubaki mwenye kukubali hukumu au maamuzi au kadri ya Mwenyezi Mungu kwa ridhiko la hali ya juu. Kubaki mwenye utii na imani ya hali ya juu kwa Mwenyezi Mungu katika hali yoyote iwayo, kubaki mwenye kuungana na Mwenyezi Mungu na kumtegemea Yeye tu na kubaki juu ya njia ya amri Zake kwa uimara. Mwenyezi Mungu anatanagza kwamba hiki ndicho kiwango cha subira ambacho kishikwapo kinamfanya mti awe mrithi wa rehema na Baraka za Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu kamwe hawapotezi waja wake waliohalisika. Wakati mtu anapotegema moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu humpokelea subira yake. Ingawaje subira haimaanishi tu kwamba mtu kukaa kimya. Bali haki za Sala lazima zitimizwe na sala hapa inamaanisha sala zilizo faridhiwa, maombi, kumuelekea Mweneyzi Mungu kwa unyenyekevu na kwa moyo wote na kuomba msaada wake. Ni mtu yule ambaye ameepukana na ubinafsi tu ndiye anayeweza kutimiza haki za sala. Mtu asiye na majivuno, kutaka sifa na kujionyesha. Sala ya mtu asiye na sifa hizi sio sala ya kweli. Mwenyezi Mungu Hamjali mtu kama huyo.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu humjali mtu yule ambaye ni mwenye unyenyekevu wa hali ya juu na pia anao uimara usiotingishika wa maungano na Mwenyezi Mungu. katika zama zetu hizi Mwenyezi Mungu akiongea na Masihi Aliyeahidiwa hususan alimwambia anazipenda njia zake za unyenyekevu. Ni njia hizi za unyenyekevu ambazo zimefungua milango mingi na mipana ya maendeleo. Iwapo mtu anataka kushiriki katika hizo, iwapo mtu anapenda kuonja ladha ya tunda la subira, iwapo naataka sala zake zikubaliwe, basi ni jambo la lazima kumuelekea Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu na uimara. Hili tu ndilo litakalotuokoa dhidi ya shetani. Hili ndilo litakalotupa nguvu na kutubariki ukaribu na Mwenyezi Mungu

Hata hivyo isifikiriwe kwamba ni jambo rahisi kushika unyenyekevu. Kuna ubinafsi mwingi, kuna uvivu (uzembe) mwingi, kuna matamanio mengi ya kidunia, hayao yote hayamwachi mtu awe mnyenyekevu; kama aya isemavyo: 'na kwa hakika jambo hilo ni gumu'. Upole na Unyenyekevu ni jambo zito sana na mambo mengi humsababishia mtu akwame njiani. Siku zote tuwe wazingativu kwamba Mwenyezi Mungu anataka watumishi wake waonyeshe subira na watekeleze ibada zao kwa kiwango ambacho hata muda mchache tu wasionyeshe kughafilika kwa kukielekea kitu kingine zaidi ya Mwenyezi Mungu. Hata hivyo Yeye mwenyewe amesema kwamba jambo hili sio rahisi na haliwezekani bila ya rehema zake. Hivyo mtu amuelekee Mwenyezi Mungu na amuombe msaada wake na hilo nalo litawezekana iwapo mtu atamwelekea Mwenyezi Mungu kwa unyenyeekvu na kwa imani kwamba 'ya kwamba watarejea kwake.

… Wakati tumwombapo Mwenyezi Mungu tuzingatie kwamba Yeye ni mwenye uwezo wa kila kitu na pia tuzingatie kwamba sisi si chochote na tunataka Atukubalie maombi yetu na aturuzuku unyenyekevu. Kisha kuna haja ya kujitahidi kuwa imara katika sala zetu. Pia tujitupe kwa Mwenyezi Mungu kuomba msamaha iwapo sala zetu, na matendo yetu mengine, au unyenyeekvu wetu wa juu juu hauna ukweli wowote, isije ikawa kinachoonekan kwa juu kuwa unyenunyekevu ikawa tu ni kujiongopea sisi wenyewe.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema: Jumuiya yetu ni lazima iwe na uzingativu wa kiasi hiki kwamba iwapo mtu atajiingiza kwenye makosa hata madogo na haijalishi yawe madogo kiasi gani kidogo kidogo yanamapeleka mtu kwenye makosa makubwa zaidi. Hatimae mapunguzu kadhaa yanamzunguka mtu huyo kiasi kwamba inamuwia vigumu kujiepusha nayo.

Binadamu, aliye kiumbe dhaifu, anajitukuza na kujiona mtukufu na mwenye sifa.

Mtu hawezi kujiokoa na mambo hayo mpaka pale atakapojihesabu kuwa si chochote na ni mnyonge na mdogo mbele ya Mwenyezi Mungu.

Bw. Kabir amesema kweli:

Imekuwa vyema kwamba tumezaliwa wanyonge na tunamsalimu kila mtu.

Ingekuwa tumezaliwa kwenye familia tukufu, ingewezekanaje kumjua Mungu

Hii ni kusema kwamba tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuzaliwa kwenye familia maskini na zilizo duni. Ingelikuwa tumezaliwa kwenye familia tajiri na zinazojihesabu tukufu, tusingepata kumjua Mungu. Wakati watu wanajitukuza kwa koo zao, Kabir anamshukuru Mungu kwa kuzaliwa kwenye koo duni.

Mtu anatakiwa kila siku ajihesabu kuwa duni na asiye chochote. Iwapo kila mtu bila kujali anatokea familia kuu kiasi gani, atatafakari juu ya udhaifu wake, kwa njia moja au nyingine, maadamu tu atakuwa atatafakari kwa umakini, bila shaka atajitambua na kujikubali kwamba yeye si chochote na hana thamani yoyote ikilinganishwa na ukubwa wa ulimwengu. Haiwezekani kwa mtu kupata njia ya kuingia kwenye ufalme wa Mungu mpaka pale atakapoonyesha utii na unyenyekevu wa kiasi kile kinachoweza kuonyeshwa na bibi kikongwe fukara, duni, mnyonge na dhaifu mbele ya mtu mkuu atokanaye na familia ya kifalme n amtu hawezi kamwe kuingia kwenye ufalme wa Mungu hadi pale atakapojiepusha na kujionesha, kutaka sifa na kiburi.

Mwenyezi Mungu aliposema kwamba '…nor will they enter Heaven until a camel goes through the eye of a needle…' (7:41). Yaani makafiri hawatofunguliwa milango ya mbingu hadi pale ngamia atakapopita katika tundu la sindano; wafasirina wengi huifasiri kwa maana ya dhahiri. Ingawaje mimi ninasema kwamba anayetaka wokovu anatakiwa azichonge hisia zake na matamanio yake katika njia za kiroho kiasi hiki kwamba aweze kupita kwenye tundu ya sindano. (kwa maana nyingine nafsi ya mtu iachane na kila ovu na kila ubaya na kila mzigo kiasi hiki kwamba ibaki tupu, ibaki nyepesi kiasi cha kuweza kupita kwenye tundu ya sindano. Wakati ambapo nafsi ya mtu itakuwa imezonga na maasi na matamanio ya kidunia haiwezi kamwe kupiata kwenye njia ile nyembamba ya kufuata sheria za kimbingu zinazopelekea kuingizwa Peponi. Hivyo lete kifo kwenye matamanio yako ya kidunia na kichonge nafsi yako kwa hofu ya Mwenyezi Mungu, ni hapo na ni hapo tu ndipo utakapoweza kupita kwenye njia ile nyembamba ambayo itakuwa ni chanzo cha uokovu wake katika maisha yajayo kwa kumfikisha kwenye Pepo. (Translated from Malfuzat, Vol. 5, pp. 437 - 439).

Mwenyezi Mungu Atujaalie kama Jamaat na Amjaalie kila mmoja wetu kama Ahmadiyya afikie kiwango cha juu cha upole na uvumilivu, wakati ambapo subira zetu zitakuwa za ukweli na uchamungu wetu utakuwa wa kweli.

Amin.

Nyota ya Kusini Imezimika

Kutoka uk. 12

mwao ni kutafuta waganga ili watoe roho yake, waganga wakajaribu na kila aliyejaribu hakufua dafu. Kila mganga aliyejaribu kutoa roho ya huyu Bwana mara wanaona amerudishanambachambilecho cha watoto wa mjini. Kila mganga anayejaribu twende! Uamuzi wa mwisho waliofikia Masheikh hao ni kuwa; "kumbe Sheikh Chilumba ndiye kiranja wa wachawi wote". Maanguko hayana mmoja.

Bwana Chilumba aliendelea bila kupata homa na Mungu Akamjaalia kupata wake wawili; Bi. Fatuma Athumani Liimbe na Bi. Amina Mohamedi Masanda. Kwa fadhila za Allah alipata watoto watano (5) na watatu kati yao ni Waahmadiyya. Bwana Chilumba amefariki tarehe 05/07/2013 akiwa na umri wa miaka 93. Wale waliomuombea kufa kwao ikabakia ni dua la kuku ambalo abadani halimpati mwewe. Wale waliomuombea asipate kizazi wakakatishwa tamaa, alipata watoto watano na watatu wakiwa ni Ahmadiyya. Jambo ambalo wanakubali watu waliomfahamu Bwana Chilumba ni kwamba katika maisha yake yote hakutetereka katika imani yake. Akiwa bado ana imani yake Chilumba alifariki tarehe 05/07/2013 na kuzikwa tarehe 06/07/2013 na sala ya jeneza iliongozwa na Mwalimu Nyenje wa tawi la Mangaka wilaya ya Nanyumbu Mkoani Mtwara. Kwa hakika sisi ni wa Mwenyezi na kwake tutarejea.



Simba wa kusini 'Chilumba' wakati wa uhai wake

Makala haya yameandikwa kwa msaada mkubwa wa Salum Dadi Mtamila na Abdallah Jabu. Jazaakumullah wa Ahsanul Jazaa.

1 Bismillahi nafungua
Kwa jina lake Jalia
Muumbaji wa dunia
Vya dhahiri na ghaibu

2 Salamu ziso idadi
Zishuke kwa Muhamamdi
Mtume wake Wadudi
Tena alo mahabubu

3 Naye wake Mfuasi
Wa ukoo wa Farisi
Twamuombea nemsi
Na matunda ya zabibu

4 Kuisha utangulizi
Nina habari ghamizi
Amefariki azizi
Chilumba ali dhahabu

5 Mohamedi wa Chilumba
Bingwa mjua kulumba
Kwa imani hakuyumba
Alitimiza wajibu

6 Maagizo ya Bayati
Ndiyo wake mlingoti
Kisoma kila wakati
Asije pata aibu

7 Msomaji magazeti
Ili kutoa ghalati
Kwake hiyo sharubati
Kadhalika na vitabu

8 Katishiwa ya uchawi
Kwake kasema hayawi
Hayawi tena hayawi
Lilikuwa lake jibu

9 Binadamu ni dhaifu
Twakuomba ya Raufu
Kila penye upungufu
Iwe sahali hesabu

10 Na pepo Firidausi
Yaillahi ya Mkwasi
Twamuombea nafasi
Chilumba wetu muhibu

11 Kaditamati watama
Muumba wetu Karima
Yarabi mpe ghanima
Ni wewe peke wahabu

Saumu Ramadhani na matatizo yetu

Kutoka uk. 12

Wanasiasa nao hawakubaki nyuma. Wameitumia vilivyo silaha hii. Baba wa Taifa la India - Mahatma Ghandi alikuwa akifunga wakati akitafuta uhuru wa India. Ingawaje yeye alikwenda mbali zaidi na kutangaza kutokula chakula hadi kilio cha uhuru kimesikika na kutekelezwa matakwa yao, anasema funga ilimsaidia sana kwani ilifanya baadhi ya mambo kuwa bayana zaidi na kumpatia nguvu zaidi za kiroho na kimwili. Nacho chama cha ukombozi nchini Tanzania TANU chini ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kilitumia silaha hii. Kiliwaomba wanachama wake wafunge saumu ili nchi ipate uhuru wake.

Kwa ujumla maelezo haya ni mahangaiko ya binadamu katika kutafuta njia iliyonyooka. Ni suna ya Mwenyezi Mungu kuwa kila nafsi yenye mahangaiko na kutafuta huoneshwa njia. Na hili ndilo chimbuko la Saumu tukufu ya mwezi wa Ramadhani.

Kwenye Qur'an Tukufu Mwenyezi Mungu Ameeleza kuwa watu kabla yetu walifunga na walikuwa na mahangaiko. Hakuna binadamu aliyefikia kilele cha mahangaiko ya kupata njia kuliko Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Hivyo yeye amepewa maelekezo yaliyokamilika juu ya saumu. Uzuri wa mafunzo ya Islam ni kwamba hayalazimishi kwa mtu bali kinachotumika ni mantiki ya jambo lenyewe. Jambo hilo linaelezwa ili ili lipokelewe si kwa lazima bali kwa kuridhika na kuwa na ridhaa ya moyo. Ukizitizama faida za saumu roho inapata shauku ya kutimiza maagizo yote kuhusu saumu. Hakuna nafsi isiyopenda kuvuna mema.

Saumu ya Ramadhani ikifuatwa kwa kiini chake ina uwezo wa kuondoa mahangaiko na taharuki, vitu ambavyo vinatupeleka puta na kuwa kama nzige waliotawanywa. Mwanadamu usiku na mchana ametawaliwa na ibada moja nayo ni kutafuta mali. Islam haijakataza kutafuta mali, lakini kufanya hiyo kuwa ndiyo shabaha ya kuja duniani kwa hakika ni msiba mkubwa. Saumu ya Ramadhani inatueleza kutumia muda mrefu katika usomaji wa Qur'an Tukufu ili tuelewe shabaha ya kuumbwa kwetu na tuelewe wajibu wetu kwa Allah na kwa viumbe Wake. Usomaji wetu wa Qur'an Tukufu unatukumbusha kuwa kulikuwepo na watu wenye nguvu na uwezo kuliko sisi na hao wote 'walipotakabari' waliangamizwa. Somo hili linasimama hadi leo. Yapo mataifa yanayodhani dunia hii wameumbiwa wao. Wanachosema wao ndiyo sawasawa. Ukitofautiana nao nongwa. Na wakitaka wanakuvamia, wanakupiga, na haya yote wanasema ni kwa faida yako.

Usomaji wa Qur'an Tukufu kwa kuzingatia unatukumbusha kuwa mchwa akiota mabawa basi fahamu anaelekea kwenye maangamizi. Kanuni hii inamkumba yeyote anayepita katika anga hizi. Kwa kuzingatia usomaji wa Qur'an Tukufu asaa binadamu akaacha kuwashambulia binadamu wengine. Maafa yanayoendelea Iraq, Afghanistan, Pakistan yanatokana na kibri na majivuno ya taifa hilo ambalo linadhani limepewa wajibu wa kuwa polisi wa dunia.

Umasikini wa kutengenezwa unadumu duniani kwa sababu ya ulafi wa watu wachache, malighafi zote zinatoka kwa Mwenyezi Mungu na ni kwa ajili ya viumbe wake wote. Wajanja wachache kwa ujanja na hila wamewafanya mamilioni kama sio malaki wakose kupata mkate wao wa kila siku. Usomaji wa Qur'an Tukufu unatukumbusha kuwa katika mali hiyo uliyo nayo kuna sehemu ya masikini. Kuwasaidia masikini sio unawafanyia ihsani, bali ni wajibu wa lazima na unasaidia kuondoa tabia ya binadamu ya kuwa mchoyo.

Lakini mwenye pupa ya mali atafahamu vipi maumivu anayoyapata yule ambaye kutwa kucha njaa ndiyo rafiki yake? Saumu ya Ramadhani inamuingiza huyo aliyo nacho katika ulimwengu wa yule ambaye hanacho. Kuelewa kitu si kwa njia ya nadharia tu, bali ni jambo la msingi katika kutenda. Huwezi kufundisha nadharia ya kuogelea bila hatimaye kumpeleka mwanafunzi baharini. Ustaadhi Saumu Ramadhani anatupeleka katika bahari ya umasikini ili angalau kwa siku nzima na mwezi mzima tuelewe mashaka wanayoyapata masikini. Huenda hilo likatusaidia nasi tukawarahisishia maisha yao ambayo Mtume Muhammad (saw) 'Ufukara ni nusu ya kufuru'.

Hali ya utowaji huduma ya afya inatisha. Kwa kiwango kikubwa huduma hii imevamiwa na matapeli. Hawajali afya ya mtu, bali fedha zako zilizo mfukoni. Ukikosea tu kwenda kuwaona utakipata 'chamtemakuni' wangelikuwa na uwezo wa kutibu labda nafuu ingepatikana, lakini hawatibu. Kielelezo chetu ni kikombe cha babu wa Loriondo, Eee Mola Tunakuomba tusinyweshwe tena kikombe hiki.

Gharama za matibabu zimekuwa kubwa mno. Katuni moja ilimuonesha bwana mmoja aliyekuwa amefumba macho, kisa palikuwa na tangazo pale hospitalini 'kumuona Daktari 20,000' huyu bwana kuona tangazo hilo akasema yote ya nini haya akafumba macho yake asimuone Daktari! Maradhi mengi yameongezeka yanatokana na vyakula na hali ya hewa. Madawa mengi yanayouzwa ni yale yaliyopitwa na wakati na hivyo badala ya kuwa dawa zinakuwa sumu. Humo mahospitalini huduma haziridhishi, uhaba wa Madaktari na uhaba wa dawa. Hali hii yote viongozi wetu hawawezi kuifahamu kwani wao wanatibiwa nje. Katika hali hii masikini ana nafasi gani ya kupata tiba? Moja ya faida ya saumu ya ramadhani ni kutibu maradhi. Wataalamu wa tiba hawana tena shaka na jambo hili. Ni dawa nzuri iliyoje saumu ya ramadhani kwa watu masikini.

Maendeleo ya binadamu yanapatikana tu kwa kutii amri za Mwenyezi Mungu. Saumu ya Ramadhani inalilemba vilivyo fundisho hili. Katika mwezi huu hata mambo yaliyo halali yanakatazwa na tunatii. Maana yake kama tuko tayari kutii na kuacha yaliyo halali seuze yaliyoharamishwa!

Saumu ya Ramadhani ni semina kuhusu utii. Na utii ndiyo jiwe kuu la pembeni la maendeleo ya nchi.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Ramadhan 1434 AH | Julai 2013 | Wafa 1392 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Asiyeachana na kuongopa na kudanganya, Mungu hana haja ya kwamba yeye mtu huyo aache chakula chake na kunywa kwake. (*Bukhari*)

Unyenyekevu na Upole ndio njia ya kumfikia Mungu - Khalifa Mtukufu

Na Mwandishi wetu

Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. katika moja ya hotuba zake za Ijumaa hivi karibuni aliwaelekeza wanajumuiya juu ya kuwa wanyenyekevu na wapole kama njia ya lazima ya kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu.
Khalifa Mtukufu alianza hotuba yake kwa kusoma aya zifuatazo:

Na ombeni msaada kwa subira na kwa Sala; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu.
Ambao wana yakini ya kwamba watakutana na Mola wao na ya kwamba watarejea kwake. (2:46-47)

Ili kufikia ukaribu na Mwenyezi Mungu mambo ya msingi ambayo aya hizi zinatufundisha, na pia aya zingine nyingi ndani ya Qurani Tukufu zinatuelekeza ni unyenyekevu / upole na kujiona si kitu (unyonge na kutokujiona muhimu). Msingi wa amri zote zilizo muhimu ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu ni unyenyekevu na upole. Au inaweza kusema kwamba kufuata amri za Mwenyezi Mungu kunanmfanya mtu afikie unyenyekevu na upole na kwa hakika sifa hizi zinzalika ndani ya dhati ya mwaminio wa kweli iwapo anafuata amri za Mwenyezi Mungu kiuhalisia. Akifafanua kauli hii: *wayaziduhuu Khushua* '…na huwazidishia unyenyekevu.' (17:110); Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema Maneno ya mwenyezi Mungu hukuza upole na kujidogosha ndani yao.



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (a.t.b.a)

Wakati mwaminio anadai kwamba anamwamini Mwenyezi Mungu na anasoma neno la Mwenyezi Mungu na kudai kulifuata katika matendo yake, kwa hakika hawezi kufikia ukamilifu wake iwapo sio mpole na mnyenyekevu au kwa maneno mengine ni kuwa mtu atakuwa tu mwaminio wa kweli pale ambapo kutokana na upole wake na unyenyekevu wake kumwabudu kwake Mwenyezi Mungu na matendo yake mengine kunafikia ukamilifu. Manabii wa Mwenyezi Mungu wamekuja kwenye dunia hii ili kutangaza kusudio hili na waliongoza kwa mifano ya maisha yao yaliyotakasika. Katika manabii wote mbora wao kabisa kwa kuonyesha mfano ni Mtukufu Mtume s.a.w.
Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema: Mwenyezi Mungu Aliyetukuka daima yu Mrehemevu na Mkarimu. Anamkuza mwanadamu kwa kila njia na anamhurumia sana. Ni kutokana na huruma na rehema zake kwamba Anawatuma Mitume na Manabii ili waweze kuwaokoa wanadamu dhidi ya maisha maovu. Ingawaje kiburi ni uovu wa hatari kabisa. Hicho kinapelekea kifo cha kiroho kwa mtu anayekiingiza ndani yake. Ninao ujuzi wa yakini kwamba uovu huo ni mbaya zaidi ya kuua.
Mtu mwenye kiburi anakuwa ndugu wa shetani kwa sababu kilikuwanikiburikilichomfanya shetani adhalilike. Hivyo ni sharti la lazima kwa mwaminio kwamba asiwe na kiburi hata chembe. Kinyume chake

Endelea uk. 10

Nyota ya Kusini Imezimika

Na Mwandhisi wetu
Dar es Salaam

Ukisikia mtu alijiunga na JumuiyyayaAhmadiyyamwaka 1956 basi elewa alikumbana na yafuatayo; kutupiwa michanga, kutemewa mate, kutukanwa, k uzomewa, tena hayo yote yakifanywa na watoto na wakubwa pia. Kutopokea salamu yako, kutotumia kisima chao waungwana kwani wewe kafiri! Kama umeoa kunyang'anywa mke, na kama unataka kuoa usipewe mke. Sokoni usiudhiwe bidhaa. Ukiwa na mzazi akutolee radhi, na ukifa usisaliwe wala kuzikwa na waislam. Ukiona mtu amevumilia yote hayo elewa vizuri ya kwamba tayari amekwishamaizi umuhimu wa ujaji wa Masihi wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Mtu wa sampuli hii anastahili heshima zetu. Usipomheshimu mtu wa namna hii hatuwezi kuelewa heshima unamuwekea nani basi!

Bwana Mohamedi Hamisi Chilumba aliyezaliwa kijiji cha Mpopo wilaya ya Masasi mwaka 1920 na k ujiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya mwaka 1956 enzi za Sheikh Fadhlullah Bashiri anastahili kukumbukwa kwani haikuwa kazi rahisi siku hizo kukiuka kuta na kuingia nyumba ya Masihi. Lakini Chilumba ambaye pia alipigana vita ya pili ya dunia mwaka 1939 - 1945 aliruka vizingiti vyote na akakutana na dhoruba kali. Akiwa Rufiji alikutana na Mwalimu Abdulkarim ambaye alimpa maelezo juu ya Jumuiyya na maelezo hayo akayaweka rohoni. Lakini hatimaye mwaka 1956 akajiunga na Jumuiyya ya Waisalam wa Ahmadiyya.

Upinzani ulikuwa mkali, yalianza mabishano ya hoja na kama ilivyo kawaida akawapiga mweleka wapinzani, akathibitisha kwa wale ambao walikuwa ni wapinzani wake kwamba utume unaendelea, kwamba Nabii Issa (as) amefariki na Masihi Aliyeahidiwa (as) si mwingine bali ni Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Kilichowachanganya wengi ni kwamba kila neno alilolitoa liliambatana na ushahidi kutoka katika Qur'an Tukufu. Mashekh wakabaki kung'aka na kufoka. Wakadai kwamba wamedhalilishwa na kwamba huyu bwana anataka kuweka kitumbua chao mchanga.

Kutokana na kushindwa huko Masheikh hao wa Kusini wakatafuta njama za kumuangamiza Bwana Mohamedi Hamisi Chilumba. Njia iliyokuja haraka vichwani

Endelea uk. 11

Saumu Ramadhani na matatizo yetu

Na Mwandhisi wetu
Dar es Salaam

Saumu kwa kiwango chocote utakacho na maana yoyote utakayotaka kimekuwa chombo muhimu katika kuwapatia binadamu fursa zaidi ya kutafakari, kuandisi na kuwa baidi na matamanio na mvuto wa mambo ya kimwili ili kupata shabaha iliyotukuka zaidi na jambo la tunu ambalo halipatikani kwa njia rahisi. Saumu inakupunguzia mahangaiko ya kufikiri kula na kunywa tu, kwani kama alivyosema Mtume wa Mwenyezi Mungu Nabii Issa (as) katu 'Binadamu haishi kwa mkate tu'.

Historia inatupa ushahidi ya kwamba wale wote walioleta mabadiliko duniani, kwa kiwango fulani walizama na kutumia silaha hii. Wale waliotaka fursa zaidi ya kufikiria jambo lililokuwa linawasumbua walikimbilia kuitumia silaha hii. Inaonesha saumu ina uwezo wa kuipa nafsi nafasi ya kutosha kupata utulivu na kuamsha mishipa ili ifanye kazi kwa kiwango kikubwa.

Napolian Bonapart yule Jenerali maarufu wa jeshi la Ufaransa alitumia wakati mwingi amefunga au tuseme kuacha kula ili afikirie zaidi maslahi ya Wafaransa. Mwandishi maarufu katika fasihi ya Kifaransa Victor Hugo ambaye umaarufu wake umesimama zaidi kwenye riwaya yake ya 'The misirable' alitumia funga iliyompatia utulivu alipokuwa akiandika riwaya yake hiyo maarufu.

Sir Isack Newton mwanasayansi maarufu yeye alifunga bila hata kufahamu kuwa amefunga! Uzito wa kazi yake ulimsahaulisha kula na kwa njia hiyo alikuwa amefunga! Inasemekana ya kwamba hata lile lile tunda lilipoanguka na kuamsha fikra zake alikuwa amekaa saa kadhaa bila kuweka riziki tumboni. Hali hii unaweza kuipa jina lolote lakini bila shaka kuna chembechembe za funga.

Endelea uk. 11